# Nipashe

Jumatatu Aprili 29, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579904

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13

UNDER THE SAME SUN

## Waitaka serikali ichukue hatua ufukuaji makaburi wenye ualbino

UKURASA 3

# Fao upotevu wa ajira sasa ndani ya siku 14

• **880** mikononi mwa polisi kughushi nyaraka kujipatia mabilioni... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli pamoja na Mkewe, Janeth Magufuli, wakimpongeza Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, Mhashamu Gervas John Mwasikwabhila Nyaisonga, baada ya kusimikwa kuwa Mkuu wa Jimbo hilo jijini Mbeya, jana. **PICHA: IKULU**

## Askofu Pengo aonya vikali ulevi wa asubuhi

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**CAG ABAINI MAPYA MIRADI YA SHULE**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kuchelewa...

**UKURASA WA 4**

**NI WIKI YA MAPROFESA NDALICHAKO, MBARAWA**

BUNGE limeingia katika wiki ya tano leo, huku wizara mbili za Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya...

**UKURASA WA 5**

**LIPUMBA AISUKA UPYA SAFU YA CUF**

CHAMA Cha Wananchi (CUF) kimewateua wanachama 13 kushika nafasi mbalimbali za uongozi ili kusaidia...


## TEC yampa tano JPM

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA, AZAM NI ZAIDI YA VITA LEO UK.32 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Askofu Pengo akemea ulevi

**Na Romana Mallya**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Kardinali Pengo, amekemea ulevi wa asubuhi, akiitaka serikali kuchukua hatua.

Askofu Pengo alitoa rai hiyo jana katika misa ya kumsimika Askofu Gervas Nyaisonga kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya.

Ibada hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwamo Rais John Magufuli, aliyeambatana na mke wake, Janeth Magufuli.

Katika misa hiyo, Askofu Pengo alisema ni serikali pekee inayoweza kuwawezesha kutamka kwa dhati kuwa haiwezekani watu kuwa wamelewa kabla ya saa tatu asubuhi.

"Serikali ndiyo inayoweza kutufanya tukaishi hivyo, kwa hiyo kusudi Roho Mtakatifu asibezwe, asisahaulike yeye ni nafsi ya pili ya Mungu, tunahitaji kanisa linaloshirikiana na serikali kuweka mazingira yanayotakiwa, kwa kanisa peke yetu hatuwezi," alisema.

Askofu Pengo aliongeza: "Hatuna mahali pa kuwachukua vijana wetu tukawaweka tukawapa nidhamu ya kutokulewa kabla ya saa tatu asubuhi."

Alisema Askofu hatakiwi kubeza shughuli inayofanywa na serikali ya kuwapa nidhamu vijana hao na kueleza kuwa kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha Roho Mtakatifu.

"Kazi iliyo njema ya kuwapa nidhamu vijana wetu ya kutokulewa kabla ya saa tatu asubuhi, ni kazi ambayo inawezekana tu kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, jambo hili ni la muhimu kwetu kulitambua," alisema.

"Mtume Petro alisimama akawaambia hebu fikiria haijafika hata saa tatu asubuhi, watu hawa wamepata wapi muda wa kulewa kwa kiwango hicho, sasa maneno hayo ya Mtume Petro yanaweza yakawa maneno halali katika mazingira yake na nyakati zile, sijui kama Tanzania ya leo tunaweza kuambizana hivyo," alisema.

INAENDELEA UK. 26

# Fao upotevu wa ajira sasa ndani ya siku 14

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umesema ulipaji wa mafao ya ukosefu wa ajira sasa unafanyika ndani ya siku 14 iwapo mwanachama amekamilisha nyaraka zote.

Vilevile, mfuko huo umesema katika ukaguzi wa nyaraka za waombaji wa fao la upotevu wa ajira kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, maombi 880 yenye madai ya Sh. bilioni 8.8 yalibainika kuwa feki.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Willium Erio, alisema kwa mujibu wa utaratibu, fao la upotevu wa ajira linatakiwa kutekelezwa ndani ya siku 30, lakini wameamua kurahisisha ili kuondoa usumbufu kwa wanachama.

Alibainisha kuwa katika kushughulikia madai ya miezi mitatu iliyopita, baadhi ya wanachama baada ya ufuatiliaji wa kina, walibainika wanadanganya kwamba hawako kazini, ilhali wako kazini.

"NSSF tumejiwekea utaratibu wa kulipa fao la ukosefu wa ajira ndani ya siku 14 baada ya mhusika kuwasilisha nyaraka zote muhimu, ikiwamo mwajiri kupeleka michango yote kwa wakati, lakini utaratibu wa kisheria ni siku 30," Erio alisema.

Fao la upotevu wa ajira kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018 ni asilimia 33.3 ya mshahara wa mhusika wakati anaachishwa kazi, na inatakiwa awe ameachishwa kazi na siyo kuacha kwa hiyari.

Alisema mafaili ya waombaji waliogushi nyaraka yamekabidhiwa kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa ajili ya kuwakamata na kuwafikisha mahakamani kwa udanganyifu na kughushi nyaraka.

"Kuna udanganyifu sana katika fao la upotevu wa ajira, hili ni tatizo la kitaifa ambalo litamalizwa na uwapo wa vitambulisho vya taifa kwa kuwa kila mmoja atakuwa na namba yake na taarifa zake zikiwekwa itaonyesha anafanya kazi wapi," alisema.

Erio aliongeza: "Mtu anakwambia ameachishwa kazi, lakini ukifuatilia yuko sehemu nyingine anafanya kazi, siyo kila anayeleta

INAENDELEA UK. 26



Wanawake wa Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya, wakisherehekea Siku ya Muungano kwa kusomba mchanga katika upanuzi wa hospitali ya Wilaya. **PICHA: IBRAHIM YASINI**

# Maaskofu Katoliki wampongeza JPM

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) limempongeza Rais John Magufuli kwa kufungua milango kwa wadau wa maendeleo na kutoa misaada kwa nchi zilizopatwa na majanga ya mafuriko na kimbunga.

Pongezi za TEC zilitolewa jana jijini Mbeya na Makamu wa Rais wa baraza hilo, Askofu Flavian Kasala, wakati wa misa ya kumsimika Askofu Gervas Nyaisonga kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya.

Katika misa hiyo Rais Magufuli alionekana akiongoza kukusanya sadaka kutoka kwa waumini.

Askofu Kasala ambaye pia ni Askofu wa Jimbo la Geita, alisema maendeleo yanahitaji mazungumzano na kusikilizana baina ya serikali na wadau.

"Hili ni hitaji muhimu katika ngazi zote za serikali. Tukiendelea kukupongeza kwa jitihada ulizochukua hadi sasa umefungua milango na kuwakaribisha wale wote walio tayari kukaa," alisema.

Askofu Kasala aliongeza: "Tunaamini siyo tu itasaidia kutatua changamoto nyingi ambazo viongozi wa dini na ngazi zote wanakubaliana nazo wakati wa kutimiza majukumu yetu ya kuwatumikia Watanzania hasa wale wanyonge, wenye kipato cha chini na maskini.

"Ni jambo jema na wataendelea kuzienzi desturi za taifa, sheria na taratibu zenye kuzingatia haki na usawa katika kuwafikia raia wote na kuwapatia watu wote huduma za maendeleo kama unavyosisitiza maendeleo hayana chama."

Askofu Kasala alimweleza Rais Magufuli kuwa wanamwombea avuke vikwazo vyote ambavyo vinaweza kuingilia juhudi zake za kuliendeleza na kulikomboa taifa.

Alisema baraza hilo linampongeza Rais Magufuli kwa kitendo chake cha kutoa msaada wa hali na mali kwa nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe zilizopatwa na maafa ya mafuriko na vimbunga.

"Tuwe karibu nao kwa misaada, tunakushukuru kwa serikali yako kupeleka msaada. Hata nchi yetu ingekumbwa lakini tuendelee kuiombea, tuendelee kumlilia na kumwomba Mungu wakati huo huo tuongeze jitihada za kuondoa majanga ya asili yale ambayo sisi tumekuwa waanzilishi wake," alisema.

Baraza hilo limelaani kitendo cha mauaji yaliyotokea Pasaka Sri Lanka na kusababisha vifo vya mamia ya watu, likieleza kuwa tukio hilo ni la ukatili ambao Tanzania inapaswa kujifunza kuwa unyama unajengeka nyuma ya chuki.

Akizungumza katika misa hiyo, Rais Magufuli alisisitiza upendo uliozungumzwa awali na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Kardinali Polycarp Pengo.

"Ninakupongeza Askofu Gervas Nyaisonga kwa kusimikwa kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, ninakujua tangu ukiwa Dodoma wakati huo tulikuwa tukisali ulipokuwa huko," alisema.

Rais Magufuli alisema wakati akiwa mdogo alitamani kuwa padri au askofu lakini ndoto zake hizo hakuzifanikisha.

"Wakati waimbaji walipokuwa wakiimba nyimbo nzuri sana zimenikumbusha sana wakati ule, nikajiuliza nilikosea wapi, yangekuwa masharti tanalegezwa ningemwomba Baba Askofu Nyaisonga niwe padri nihubiri neno la Mungu ambalo ni muhimu katika maisha ya dunia," alisema.

Rais Magufuli alisema uaskofu ni daraja takatifu na ni wito kutoka kwa Mungu na ni kazi ngumu.

"Kazi ya uaskofu ni kazi ngumu, leo (jana) tunakushangilia lakini kadri tunavyokushangilia shetani anachukia, najua aliyekuchagua ni Mungu atakufikisha salama kuliongoza gurudumu la Jimbo Kuu Mbeya," alisema.

Rais Magufuli aliwaomba viongozi wa dini waendelee kuliombea taifa ili liendelee kukua kiuchumi na kuepukana na majanga mbalimbali.

Naye Askofu Nyaisonga alishukuru kwa namna ambavyo makundi mbalimbali yalishiriki kumsaidia kimwili na kiroho hadi kufika hatua hiyo.

***Imeandikwa na Nebart Msokwa (MBEYA) na Romana Mallya (DAR)**

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifurahia jambo na watalii kutoka Israel, kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa KIA. Kushoto ni Naomi Moscovich, akiwa na binti zake, Dana Moscovich (kulia) na Lihi Moscovich (katikati). **PICHA: OWM**

# Waitaka serikali ichukue hatua ufukuaji makaburi wenye ualbino

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Kutetea Watu Wenye Ualibino la Under The Same Sun, limeomba serikali kuchukua hatua kukabiliana na changamoto ya ufukuaji wa makaburi ya marehemu waliokuwa ualbino.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mragibishi wa shirika hilo, Kondo Seif, alisema watu wenye ualbino walioko hai wako hatarini ingawa sasa wengi wao wanahifadhiwa kwenye vituo maalum.

"Kuna wenye ualbino kama mwanadamu wa kawaida inafikia mahali unapoteza maisha unazikwa, wakati wa uhai wako haukuwa salama na sasa hata ukifariki mabaki ya mwili nayo hayako salama tena kwa kuwa wanafukua na kuondoka na viungo hivyo," alisema.

Kwa mujibu wa Kondo, wamepata taarifa kuwa usiku wa kuamkia Aprili 23, mwaka huu, kaburi la Amani aliyekuwa mkazi wa Kijiji cha Ibililo mkoani Mbeya, lilifukuliwa na mabaki ya mwili wake yakachukuliwa.

"Mwishoni mwa mwaka jana, kuna ndugu wa Katibu wa Umoja wa Wenye Ualibino mkoani Mbeya, ambaye alifariki miaka mingi, kaburi lake lilifukuliwa na mabaki yote kuchukuliwa," alisema.

"Badala ya mauaji, sasa kuna suala la kufukua makaburi ya wenye ualibino, tunaiomba serikali na jamii kukemea jambo hili kwa kipindi hiki tunachoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ambako mara nyingi matukio haya huongezeka," alisema.

INAENDELEA UK. 5

# Waziri aipa maagizo TPDC gesi asilia

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kuwatumia viongozi wa serikali za mitaa ili wakawahamasishe wananchi waweze kutoa maeneo yao kwa ajili ya upitishaji wa miundombinu ya gesi asilia.

Pia, amelitaka shirika hilo kuhakikisha katika kipindi cha miaka miwili robo ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wawe wameshaunganishwa na mfumo wa utumiaji wa gesi asilia.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya ukaguzi wa usambazaji wa miundombinu ya gesi asilia katika maeneo ya Mikocheni, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), pamoja na Mlalakua.

"Watumieni viongozi wa serikali za mitaa ili waweze kuwahamasisha wananchi wao waweze kujiunga na matumizi ya gesi asilia, pia waweze kutoa maeneo yao ili miundombinu hiyo ipite kwa urahisi, Pia nataka ndani ya miaka miwili robo ya wakazi wa Dar es Saalam wawe wanatumia gesi asilia kwenye makazi yao," alisema Dk. Kalemani.

Kadhalika, Dk. Kalemani aliitaka TPDC kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kazi ya usambazaji wa gesi asilia kwenye makazi ya watu iende kwa haraka na kumalizika kwa wakati, na kueleza kuwa mkakati wa serikali ni kusambaza huduma hiyo katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Lindi, Mwanza, Kigoma baada ya miaka mitano ijayo.

"Tunataka wateja zaidi ya 1,000 wawe wameunganishwa hadi kufikia mwakani, katika eneo la Mikocheni tunataka idadi kubwa ya wananchi wawe wanatumia gesi, hakikisheni mabomba la gesi ya Ubungo Maziwa, Mlimani na Mikocheni yanaanza kusambaza gesi kwa wakazi husika," alisema Dk. Kalemani.

Alisema serikali imeshatenga Sh. trilioni moja kwa ajili ya kusambaza gesi asilia kwa wananchi, na kwamba mikakati iliyopo ni kusambaza gesi katika viwanda vyote vya Jiji la Dar es Salaam, na kwa sasa imeanza na

INAENDELEA UK. 26

# CAG abaini kuchelewa miradi shule

**Na Enock Charles**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kuchelewa kukamilika kwa miradi ya ujenzi ya shule tatu za sekondari zikiwamo Ihungo na Jangwani, yenye thamani ya Sh. bilioni 12.907.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, CAG Assad anasema amebaini kuchelewa kwa miaka hadi miwili katika kukamilisha miradi hiyo.

"Ukaguzi wa shughuli za ujenzi zilizotekelezwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, ulibaini ucheleweshaji mkubwa wa hadi miaka miwili katika kukamilisha miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. 12,906,655,213 kwa shule tatu za sekondari," Prof. Assad anabainisha.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad anabainisha kuwa uchelewaji huo ni kinyume cha makubaliano ya mkataba kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia na Wakala wa Ujenzi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule hizo.

Mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu

INAENDELEA UK. 26




# Ni wiki ya maprofesa Ndalichako, Mbarawa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeingia katika wiki ya tano leo, huku wizara mbili za Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Maji zikipangiwa siku tano za Wabunge kuchangia mjadala wa hotuba ya makadiro ya mapato na matumizi ya mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa ratiba ya Mkutano wa 15 wa Bunge la bajeti iliyotolewa na Ofisi ya Bunge jijini Dodoma kuanzia Aprili 23 hadi Juni 28, mwaka huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndiyo itakayoanza kuwasilisha bajeti yake leo na kujadiliwa kwa siku mbili mfululizo. Ratiba hiyo inaonyesha kuwa chombo hicho muhimu cha kutunga sheria, kitajadili bajeti ya Wizara hiyo kati Aprili 29 na Aprili 30, mwaka huu.

Wakati Wizara ya Maji itawasilisha bungeni hotuba yake ya makadirio na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20 kuanzia Mei 2 hadi Mei 6 mwaka huu Bunge hilo litakapohitimisha mjadala wa wizara hiyo.

Mjadala wa wizara hiyo ulipangwa kuchukua siku tatu ambapo wabunge wanatarajiwa kueleza changamoto za maji zinazowagusa wananchi wengi katika maeneo mengi nchini.

Mei 7 hadi 8, Bunge pia litajadili hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa siku mbili mfululizo.

Pia itajadili hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa siku tatu ambayo ni kuanzia Mei 10 hai Mei 13, mwaka huu.

# Serikali yabeba wakulima pamba

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SERIKALI imewaahidi neema wakulima wa pamba nchini, ikisema itawawezesha kwa zana bora ili kuongeza uzalishaji.

Mpango huo wa serikali ulitangazwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Inocent Bashungwa, akisema kwamba wizara hiyo itahakikisha inawasaidia wakulima zana bora za kilimo cha pamba ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 400,000 mwaka 2018/2019 hadi tani 1,000,000 mwaka 2020/2021.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano wa 15 wa sekta ndogo ya pamba uliofanyika jijini Mwanza.

"Wizara yangu itahakikisha inawasimamia wakulima wa pamba kuwapatia zana bora na za kisasa za kilimo zitakazowawezesha kuzalisha pamba kwa wingi pamoja na kuwapatia pembejeo za kilimo, viatilifu vya kuua wadudu waharibifu ili kuongeza uzalishaji na kufikia malengo," alisema Bashungwa. Bashungwa alisema katika msimu uliopita wa ununuzi wa zao hilo (2018/2019) uzalishaji ulifikia tani 222.039 zilizozalishwa msimu wa 2017/2018, hivyo kukubali kulifufua kwa nguvu zote zao la pamba ambalo lilikuwa limekufa miaka ya nyuma. Mkutano huo uliwashirikisha wadau mbalimbali wa pamba, wakurugenzi wa bodi ya pamba,

wakuu wa mikoa yote inayolima zao hilo, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri za wilaya, wenyeviti wa halmashauri za wilaya, vyama vya msingi vya ushirika ,wabunge na wakulima wa zao hilo.

Bashungwa alisema katika mkutano huo alikwenda kupata maoni ya wadau wa pamba na wakulima kuhusu namna ya uendeshaji wa kilimo hicho kwa kutumia mfumo wa kisasa wa uzalishaji wa zao hilo, huku akiwaonya watendaji watakaojaribu kufanya hujuma katika kilimo hicho, watachukuliwa hatua za kisheria.

Canara Bank (Tanzania) Ltd.

Together we can build a better life

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2019 | Robo Mwaka uliopita 31 Desemba 2018 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 564.19 | 719.43 |
| 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 5,380.54 | 4,529.93 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 26,312.24 | 22,747.68 |
| 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,492.33 | 754.13 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 119.42 | 93.33 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 28,580.12 | 36,089.07 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 31,786.22 | 34,838.56 |
| 12 Mali Nyingine | 1,171.88 | 1,559.20 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 886.37 | 946.37 |
| **16 JUMLA YA MALI** | 97,293.31 | 102,277.70 |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 30,859.73 | 37,602.23 |
| 18 Amana za Wateja | 30,718.77 | 28,960.70 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 6.10 | 7.51 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 924.46 | 1,100.49 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| 27 Dhima Nyingine | 37.84 | 111.80 |
| 28 Madeni | 0.00 | 0.00 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | 62,546.90 | 67,782.73 |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | 34,746.41 | 34,494.97 |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 463.10 | 539.29 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 1,201.87 | 234.14 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 251.44 | 891.54 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 0.00 | 0.00 |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **34,746.41** | **34,494.97** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 13,772.00 | 4,497.06 |
| 39 Mikopo Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 161.27 | 101.27 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 35.71% | 33.73% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.00% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 51.88% | 52.49% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 32.84% | 34.16% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.65% | 92.33% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -7.49% | 5.91% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -4.87% | 4.12% |

**Notisi**

*Mikopo Ghafi=Mikopo Halisi+Bili zilizoafikiwa+Tengo kwa ajili ya mikopo chefuchefu

*Jumla ya Amana = Amana za wateja + Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha + Amana Maalum+ Madeni

*Mali zenye riba = Uwekezaji katika amana za serikali + Mikopo Halisi +bili zilizoafikiwa+mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine + salio katika benki nyingine

* BENKI IMEANZA OPARESHENI 09 MEI 2016.

### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2019

| | Robo ya mwaka sasa 31 Machi 2019 | Robo ya mwaka linganishi(mwaka uliopita) 31 Machi 2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2019 | Limbikizo la mwaka linganishi(Mwaka uliopita) 31 Machi 2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 1,836.15 | 1,447.20 | 1,836.15 | 1,447.20 |
| 2 Gharama za Riba | 541.05 | 467.80 | 541.05 | 467.80 |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | 1,295.10 | 979.40 | 1,295.10 | 979.40 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 60.00 | 50.00 | 60.00 | 60.00 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba** | 195.09 | 166.38 | 195.09 | 166.38 |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha | 51.18 | 22.16 | 51.18 | 22.16 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 143.91 | 144.22 | 143.91 | 144.22 |
| 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | 1,058.75 | 902.33 | 1,058.75 | 902.33 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 337.26 | 296.40 | 337.26 | 296.40 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 721.49 | 605.93 | 721.49 | 605.93 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | 371.44 | 193.45 | 371.44 | 183.45 |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 120.00 | 45.00 | 120.00 | 45.00 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 251.44 | 148.45 | 251.44 | 138.45 |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 20 | 16 | 20 | 16 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 8 | 5 | 8 | 4 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 8 | 5 | 8 | 4 |
| 14 **Idadi ya Matawi** | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.25% | 0.17% | 1.01% | 0.68% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.73% | 0.44% | 2.91% | 1.76% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 52.12% | 55.92% | 52.12% | 55.92% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.64% | 5.20% | 5.64% | 5.20% |

*Ada na kamisheni inahusisha ada ya wakaguzi,kodi na ada ya leseni na Bima

* uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali=mapato halisi kabla ya kodi/wastani wa mali

*Mapato Ghafi =Mapato yasiyo na riba +Mapato ya riba

*Wastani= (opening +closing)/2

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA 31 Machi 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni )

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2019 | Robo Mwaka iliyopita 31 Desemba 2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2019 | Limbikizo la mwaka linganishi(Mwaka uliopita) 31 Machi 2018 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 251.43 | 209.31 | 251.43 | 148.45 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Hasara katika mali | 240.00 | 324.82 | 240.00 | 172.00 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 3,052.34 | -7,510.34 | 3,052.34 | -6,200.52 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mabadiliko halisi katika Amana | -4,984.43 | 3,714.47 | -4,984.43 | 11,478.17 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | -242.34 | 124.16 | -242.34 | 300.08 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 181.23 | -26.38 | 181.23 | -402.55 |
| Kodi iliyolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | -1,501.77 | -3,163.96 | -1,501.77 | 5,495.63 |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | -6.75 | -33.73 | -6.75 | -43.97 |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (3,564.55) | 701.38 | (3,564.55) | 1,566.55 |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji | -3,571.30 | 667.65 | -3,571.30 | 1,522.58 |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mengineyo(bainisha) | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | -5,073.07 | -2,496.31 | -5,073.07 | 7,018.21 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 42,092.56 | 44,588.87 | 42,092.56 | 34,649.74 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka | 37,019.49 | 42,092.56 | 37,019.49 | 41,667.95 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 1125.67 | 45.93 | 493.37 | 0.00 | 34,494.97 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0.00 | 0.00 | 251.44 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 251.44 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Miamala na wanahisa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Gawio lililolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ziada ya Kisheria | 0.00 | 0.00 | 45.93 | -45.93 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0.00 | 0.00 | 30.27 | 0.00 | -30.27 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 1,453.31 | 0.00 | 463.10 | 0.00 | 34,746.41 |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 289.00 | 0.00 | 510.00 | 0.00 | 33,629.00 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0.00 | 0.00 | 148.45 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 148.45 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Miamala na wanahisa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Gawio lililolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ziada ya Kisheria | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0.00 | 0.00 | 50.00 | 0.00 | -50.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 487.45 | 0.00 | 460.00 | 0.00 | 33,777.45 |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| SESHAGIRIDAS H (Ofisa Mtendaji mkuu) | (Imesainiwa) | 16.04.2019 |
| PETER JONATHAN MKANDE (Mkuu wa fedha) | (Imesainiwa) | 16.04.2019 |
| ZABLON GEORGE STAMBULI (Mkaguzi mkuu wa ndani) | (Imesainiwa) | 16.04.2019 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. PATRICK AMBWENE MUWOWO DIRECTOR | (Imesainiwa) | 16.04.2019 |
| 2. RAJAB SELEMENI KAKUSA DIRECTOR | (Imesainiwa) | 16.04.2019 |

Canara Bank (T) Ltd

Head Office Dar Es Salaam Branch

Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania

E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532

www.canarabank.co.tz

215195402

## HABARI KITAIFA

# Lipumba asuka safu mpya CUF

Na Mary Geofrey

CHAMA Cha Wananchi (CUF), kimewateua wanachama 13 kushika nafasi mbalimbali za uongozi ili kusaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, aliwaeleza waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa, wameteua wanachama ambao miongoni mwao ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Aliwataja walioteuliwa ni Zaynab Amir Mndolwa, Mkurugenzi wa Fedha na Omary Mohamed Omary, ambaye atakuwa Naibu Mkurugenzi.

Wengine ni Mohamed Habibu Mnyaa, atakayekuwa Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Bunge na Sera na Mohamed Ngulangwa atakayekuwa Naibu Mkurugenzi na Mneke Jafar Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi na Mohamed Vuai Makame atakayekuwa Naibu Mkurugenzi.

Prof. Lipumba alisema wengine ni Abdul Juma Kambaya, Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma na Mbarouk Seif Salim Naibu Mkurugenzi.

Alisema kuwa Haroub Mohamed Shamis kuwa Mkurugenzi wa Haki za Binadamu na Salvatory Magafu kuwa Naibu Mkurugenzi.

Pia wamo Thinney Juma Mohammed kuwa Mkurugenzi wa Mafunzo na Uhamasishaji na Masoud Omary Mhina kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mafunzo na Uhamasishaji na Yusuph Mohamed Mbugiro aliyeteuliwa kuwa Ofisa Tawala wa Ofisi Kuu ya Dar es Salaam.

Kadhalika, Prof. Lipumba ameteuwa viongozi wa Jumuiya ya Vijana wa (CUF- JUVCUF) pamoja na Jumuiya ya Wanawake (JUKECUF)

Hata hivyo, alisema kwa upande wa JUVCUF Kaimu Mwenyekiti ni Hamidu Bobali, Kaimu Makamo Mwenyekiti Faki Suleiman Khatib, Kaimu Katibu Mtendaji, Yusuph Kaiza Makame na Kaimu Naibu Katibu Mtendaji, Mbaraka Ismaili Chilumba.

Pia alisema JUKECUF Kaimu Mwenyekiti ni Dhifaa Mohamed Bakar, Kaimu Makamo Mwenyekiti, Kiza Husein Mayeye, Kaimu Katibu Mtendaji, Anna Ryoba Paul pamoja na Kaimu Naibu Katibu Mtendaji, Leila Jabir Haji.

"Uteuzi huu umefanywa na Mwenyekiti wa CUF kwa kushauriana na Makamu Mwenyekiti na uteuzi huu utafikishwa mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa," alisema Prof. Lipumba.

# Waitaka serikali ichukue hatua

INATOKA UK. 3

Kondo pia alisema watu wenye ualibino wana haki ya kuchagua na kuchaguliwa kama raia wengine wa Tanzania, lakini hawawezi kufanya hivyo kama hali ya usalama itakuwa duni dhidi yao.

"Tunatoa wito kwa serikali na jamii, kila mmoja awe salama katika nchi ambayo ni kisiwa cha amani na inasifika duniani, iwe salama kwa kila mmoja wetu," alisema.

Kondo pia aliipongeza serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua kwa kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wanaobainika kufanya ukatili dhidi ya wenye ualbino.

"Kinachofanya matukio haya yanajirudia ndani ya muda mfupi ni kwa sababu serikali na jamii hazijasimamia elimu kwa umma, watu wengi wanashangaa baba na mama ni weusi lakini wamezaa mtoto mwenye ualibino, ni kwa sababu hawajui -- wanatengeza dhana mbalimbali kama ni mashetani, hawana thamani yoyote," alisema.

Alisema ni vyema serikali ikafanya jitihada za makusudi kuendesha elimu kwa umma kitaifa ili watu wajue sababu za mtoto kuzaliwa na ualibino na changamoto zake na nini jamii ifanye kuzitatua.

"Tunapendekeza elimu ya ulemavu na ualibino iingizwe katika mtaala wa shule ili wanafunzi wajifunze na kujua nini kinachoendelea," alisema.

Mauaji ya albino nchini yalishika kasi mwaka 2006, na watu 19 walihukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2015.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014

CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania

1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

NOTE:
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:
a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.
b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

Note:
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)
a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)

The medium of communication is both English and Kiswahili.

12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk

DISCLOSURE UNDER REGULATION 11 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014
MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES/FEES/PRODUCTS AND SERVICES

| | CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | D. REMITTANCES | | |
| A. SAVINGS BANK | | | | TZS | USD |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 2. E Remittances | | |
| 3. A/C Statement Charges | | | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| a) Monthly | FREE | FREE | 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 | 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free Above 5000 - 0.3% | 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE | 3. SWIFT | Swift Inward | Swift Outward |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 | a) Swift Outward | | |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 | Upto 5,000 | $ 12 | $45 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 | 5,001 to 10,000 | $ 18 | $60 |
| B. CURRENT ACCOUNT | | | above 10,000 | $ 30 | $90 |
| | | | E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000 5Mio to 10 Mio – 200 T 10 Mio to 25mio – 400 T 25 mn to 500 mio - 1.5% >500mio--1.25% Min 7.5 M | Upto 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500 T–1.25% Min 7,500 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300 T | Upto 50,000 --NIL– >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly b) Interm | **5000 5000+500 for each page** | **$5 $ 5+1 for each page** | 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000 5 Mio to 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *minimum 9000 |

**Deposit Rates - In Local Currency TZS Savings A/c 2.5%**

| Amount in TZS (Mio) | 31 to 90 days | 91 to 180 days | 181 to 364 days | 1 to 2 yrs. | Above 2 Yrs. |
|---|---|---|---|---|---|
| Upto 10 Mio | 4.00 | 5.50 | 6.50 | 7.50 | 8.00 |
| 10 Mio to 100 Mio | 5.00 | 6.00 | 7.00 | 7.75 | 8.25 |
| Above 100 Mio | 5.00 | 6.00 | 7.00 | 8.50 | 9.00 |

**Deposit Rates – In Foreign Currency USD Savings A/c 0.5%**

| Amount in USD | 31 to 90 days | 91 to 180 days | 181 to 364 days | 1 to 2 yrs. | Above 2 Yrs. |
|---|---|---|---|---|---|
| Up to 5000 | 0.50 | 1.00 | 2.0 | 2.25 | 2.50 |
| 5000 TO 50000 | 1.00 | 2.0 | 2.25 | 2.75 | 3.00 |
| Above 50,000 USD | 1.50 | 2.25 | 2.75 | 3.00 | 3.50 |

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd**

| | |
|---|---|
| - Current and Saving Account | - Mortgage Loan |
| - Salary Account | - Personal Loan |
| - Student Account | - Insurance Premium Funding |
| - Fixed Deposit Account | - Safe Deposit Lockers |
| - Re Investment Deposit Account | - All Export and Import Related transactions |
| - Recurring Deposit Account | - Letter of Credit and Guarantees |
| - Overdraft and Term Loans | - E- Remit Facility to India |
| - Vehicle Loan | - Mobile Banking |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE ABOVE 25 MIO–0.12% | Upto 5000 Free 5000 to 10,000 - 0.3% Above 10,000 - 0.5% | 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25 >50,000 ---50 |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE ABOVE 50 MIO–0.12% | **Upto 10,000- Free > 10,000- 0.3%** | **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| 6. Balance Confirmation charges | 25,000.00 | $15 | Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | |
| 7. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 | Opening commission | 1.2% ( Min $ 200) | |
| 8. Cheque Return Charges | | | LC amendment Commission | 0.4% ( Min $50 max 350) | |
| a) Inward | 1500/30,000 | $1/ $15 | Swift charge for LC opening | $40 | |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 | Swift charge for other message | $40 | |
| 9. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 | Extensions - Commissions | 1.2% ( Min $200) | |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | LC cancellation charges | 1.2% ( Min $200) | |
| 1. Cash Withdrawal | | | Non payment of Bills on due date | 16% Till Payment | |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA | **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA | Advising commission | $140 | |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA | Confirmation Commission | 0.5% ( Min $150) | |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA | Negotiating bills under LC | 0.5%(Min $75+cuourier+int) | |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA | Reimbursement claim paid | 0.5% ( Min$75) | |
| 2. Funds Transfer/Mobile Wallet | | | Extensions - Commissions | 1.2% ( Min $200) | |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA | Collection of Export LC | 0.5%(Min $75+cuourier+int) | |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA | Amendments | $75 | |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA | **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA | Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA | with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter | 40% of actual charges |
| A) Monthly Subscription Charge | 500 | NA | | | |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA | | | |
| **H. LOCKERS RENT YEARLY** | | | INTEREST RATES ON LOANS AND ADVANCES | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | | TANZANIA SHILLINGS | BPLR – 16.00% MAXSPREAD 7.00% | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | | UNITED STATES DOLLARS | BPLR - 7.00% MAXSPREAD 7.00% | |
| 3. BIG | 750,000.00 | | | | |

215195501



Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O.Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D) +255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

Access your A/c 24x7

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga msifanye makosa uchaguzi mkuu Jumapili

**BAADA** ya vuta nikuvute ya muda mrefu, hatimaye mchakato wa uchaguzi mkuu wa Klabu ya Yanga umekamikika na sasa utafanyika Jumapili jijini Dar es Salaam.

Kufanyika kwa uchaguzi huo kumekuja baada ya viongozi wote kujiuzulu, hivyo Jumapili wanachama watakuwa wakichagua viongozi wapya watakaobeba jukumu la kuhakikisha Yanga inapata mafanikio katika kipindi chao uongozini.

Katika uchaguzi huo utakaosimamiwa na Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), nafasi zinazogombewa ni ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa kamati ya utendaji.

Hakika hii ni nafasi pekee kwa wanachama wa Klabu ya Yanga kutumia haki yao kikatiba kuchagua viongozi makini wanaoamini wanaweza kuiwezesha kupiga hatua moja mbele zaidi kutoka hapo ilipo.

Kama ambavyo tulishuhudia mchakato wa uchaguzi wa watani zao, Simba ukifanyika kwa amani mwaka jana hadi kufikia hatua ya kubadili mfumo wa uendeshaji na kuwa wa hisa, ndivyo ambavyo tunatamani kuona hali ikiwa hivyo kwa Yanga.

| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **4,953** | **(2,816)** | **4,953** | **22,220** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | 12 | (60) | 12 | (286) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 1 | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **12** | **(60)** | **12** | **(286)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,647 | (13,691) | 1,647 | (7,519) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **1,647** | **(13,691)** | **1,647** | **(7,519)** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **6,612** | **(16,566)** | **6,612** | **14,416** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 25,917 | 42,483 | 25,917 | 66,878 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **32,529** | **25,917** | **32,529** | **81,294** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 Decemba 2018
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2019 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 41 | - | - | - | 41 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | | | | | | |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,527) | - | 402 | - | 18,399 |
| Mwaka uliopita 2018 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,454) | - | 351 | - | 21,421 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (3,048) | - | - | - | (3,048) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (51) | - | - | - | (51) |
| Mengineyo | - | - | (16) | - | 51 | - | 35 |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |


| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Chris Byaruhanga<br>**Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu** | ***Imesainiwa*** | ***29th April 2019*** |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | ***29th April 2019*** |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | ***29th April 2019*** |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | General Robert Mboma (Rtd)<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | ***29th April 2019*** |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | ***29th April 2019*** |

215198202

UBA Africa's global bank



# PM kuzindua maabara ya kisasa ya Atomiki

**Novatus Makunga,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuzindua maabara ya kisasa ya kwanza, katika ukanda wa Afrika, iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 8.38 iliyojengwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, jijini Arusha.

Aidha, Majaliwa atafungua mkutano wa wataalam wa mionzi kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC), utakaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC).

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki nchini, Prof. Lazaro Buzagala, alisema mjini hapa jana kuwa, maabara hiyo imejengwa kwa fedha za ndani kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni mbili.

Alisema kuwa Umoja wa Ulaya (EU), umefadhili bila ya masharti yoyote kwa Serikali ya Tanzania vifaa na mafunzo kwa wataalamu watakaosimamia maabara hiyo kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni sita.

Prof. Buzagala alisema maabara hiyo itatoa huduma katika nchi za Jumuia ya Afrika ya Mashariki (EAC) na nchi za SADC.

Alisema lengo kuu la Serikali ya Tanzania kujenga maabara hiyo, ni kuimarisha zaidi udhibiti wa mionzi na pia kuimarisha matumizi ya Sayansi na teknolojia nchini na katika mataifa ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

" Lengo kuu la maabara hiyo ni kuhakikisha panakuwapo na usalama kwa wananchi wa Tanzania na mataifa mbalimbali barani Afrika, kuhusu udhibiti wa madhara ya mionzi," alisema Prof. Buzagala.

Alisema dhamira ya Serikali ya Tanzania kuunda Tume ya Nguvu za Atomiki ni kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya nishati ya Nyuklia, kwa misingi ya kuhakikisha mionzi haileti madhara kwa watumiaji.

Aidha, Prof. Buzagala, alisema pia kuendeleza matumizi salama ya Sayansi na Teknolojia ya Nyuklia, kwa kuzingatia sheria na kuhakikisha panakuwapo na maendeleo endelevu nchini.

Hata hivyo, Prof. Buzagala alisema kwa miaka mingi Tanzania ilikabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa maabara ya kisasa, kama hiyo itakayozinduliwa na Waziri Mkuu Majaliwa.

Alisema kutokana na kutambua umuhimu wa maabara hizo, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, inaendelea kufungua ofisi za kanda na maabara ndogo ndogo na hadi sasa zaidi ya maabara ndogo 20 zimefunguliwa, kwa ajili ya kupimia mionzi jambo ambalo limesaidia kupunguza malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara.

Alisema Tume inatarajia kujenga ofisi zake mjini Dodoma, Zanzibar na Mwanza, zitakazokuwa na maabara kwa ajili ya kupeleka huduma karibu na wananchi. Prof. Buzagala alieleza kwamba maabara hiyo ya kisasa na ya aina yake Afrika ina manufaa makubwa katika kipindi hiki ambacho serikali ipo katika mkakati wa kuifanya Tanzania ya Viwanda.

Alisema maabara hiyo itaimarisha kazi za udhibiti wa madhara yanayoweza kutokea kutokana na mionzi na hivyo kuwaweka Watanzania katika hali ya usalama zaidi.

Pia Prof. Buzagala alisema maabara hiyo itadhibiti na kusimamia vyema uchimbaji, uchakataji na usafirishaji wa madini ya urania na madini mengine hatarishi yatokanayo na mionzi ili wananchi wasipate madhara.

"Maabara hii itasaidia kufanya utafiti za kisayansi na teknolojia zenye hadhi ya kimataifa kwa kushirikiana na vyuo vikuu, taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania, kwa lengo la kukuza sekta ya Sayansi na Teknolojia," alifafanua.

# Magara waomba uongozi kuchunguza ubadhirifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAKAZI wa Kijiji cha Magara, wilayani Babati mkoani Manyara, wameuomba uongozi wa wilaya hiyo kuchunguza ubadhirifu wa Sh. milioni 45 wa ujenzi wa matundu 20 ya vyoo vya shule na Sh. milioni 103 zilizotolewa na mradi wa kuhifadhi mazingira Juhibu. Mmoja kati ya wakazi wa kijiji hicho, Juma Rajab, akizungumza juzi alidai wanaomba uongozi wa wilaya ufike kijijini hapo au ulete wakaguzi, kwa kuwa fedha nyingi zimefujwa na wakihoji wanakamatwa.

Alisema baada ya kufanyika mkutano mkuu wa kijiji hivi karibuni na viongozi hao kutoa taarifa potofu ya mapato na matumizi, yeye na wenzake wanne walipinga na walikamatwa na kufikishwa polisi.

Aliwataja wenzake waliokamatwa baada ya kupinga taarifa hiyo kuwa ni John Samson, Azaria Daudi, Polaa Juma na Omary Ramadhan na badala ya kufikishwa kituo cha polisi Magugu, walipelekwa Mjini Babati.

"Kuna ufujaji wa fedha umefanyika na tukipinga tunakamatwa ila tunaushukuru uongozi wa CCM Wilaya ya Babati, ambao waliingilia kati hadi tukaachiwa, wachunguzwe fedha zetu zimeliwa," alidai Rajabu.

Alidai kuwa awali waliambiwa mradi wa ujenzi wa vyoo vya Shule ya Msingi Magara, wenye matundu 20, utagharimu Sh.milioni 38, lakini baadaye wakaelezwa umetumia Sh. milioni 45.

Alidai kuwa gharama ni kubwa kwa kuwa mchanga, mawe yapo karibu na wananchi walitumia nguvu kazi zao kujenga vyoo hivyo, lakini fedha hizo wanazotajiwa ni nyingi na walipopinga, walikamatwa.

"Tunamuomba mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, afike kwenye kijiji chetu au atume mkaguzi wa ndani wa halmashauri ya wilaya, kwani hawa viongozi wamefuja fedha zetu," alidai Rajabu. Alidai pia kuna ufujaji wa fedha za mradi wa vijiji 10 vya uhifadhi wa mazingira wa Juhibu, ambazo kwa mwaka zilipokelewa Sh. milioni 103 ambazo baadhi yake zimefujwa na viongozi.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kijiji hicho Twaha Ramadhan, akizungumza kwa njia ya simu alikanusha madai hayo na kutaka mwandishi wa habari hizo, kufika ofisini kwake kuliko kuzungumza kwenye simu.


Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, alisema baada ya watu hao kukamatwa walichunguza wakakuta ni majungu hivyo wakawaachia.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema atafika kijijini hapo na kuitisha mkutano mkuu kwa lengo la kusikiliza changamoto hizo na kisha kupatiwa ufumbuzi.


**UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES**

| S/N | ITEM/TRANSACTION | RETAIL | CORPORATE |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | | |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 15,000 USD 15 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges | | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 10 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | 3 | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | SMS Alert Fee per tranx | TZS 200 | |
| | Online PASSCODE reset Fee | TZS 1500 | |
| | POS purchase | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 | N/A |
| | POS: International Tranx | 3% MINIMUM 6000 TZS | 3% MINIMUM 6000 TZS |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 15,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 15,500 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 15,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | WEB transaction (domestic) | Nill | |
| | Web Transaction Fee (International) | 3% MINIMUM 6000 TZS | |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM: OFF-US Fee (Domestic) | TZS 2,500 | |
| | ATM balance inquiry (local) | TZS 200 | |
| | ATM balance inquiry (international) | TZS 1000 | |
| | ATM: WITHDRAW Fee (International) | 3% MINIMUM 6000 TZS | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | **Soiled notes** | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | **Coins** | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **Approved by:** | | |
| | **Signature:** | **Signature:** | |
| | | | |
| | Usman Isiaka | Flavia Kyanga | |
| | **Managing Director/CEO** | **Act.Chief Operating Officer** | |
| | **United Bank For Africa (Tanzania) Ltd** | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | |

215198202





# Vijana wa Rombo watakiwa kutekeleza kazi za JPM

**Na Paul William,** ROMBO

VIJANA katika Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro wametakiwa kuhakikisha wanaunganisha nguvu zao kwa pamoja ili kupeleka mbele maendeleo pamoja na kuunga mkono kazi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dk. John Magufuli.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), kupitia Mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Tadayo, katika bonanza maalum lililoandaliwa na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Wilaya ya Rombo ikiwa ni maadhimisho ya sherehe za Muungano wa Tanzania.

Tadayo alisema kuwa, Rombo ni miongoni mwa wilaya ambazo vijana wamekuwa wakipewa kashfa za ulevi na kushindwa kufanya kazi, lakini alishangaa kuona jinsi vijana wa wilaya hiyo walivyo na nguvu kubwa.

"Mimi nilikuwa nikisikia Rombo hakuna vijana, wote wametekwa na pombe sasa nikawa najiuliza je, hawa vijana ninaowaona hapa wanatoka wapi? Ndipo nimeamini sasa maneno yale hayana ukweli wowote bali ni kwa lengo la kuwachafua tu, na kuanzia sasa natangaza Rombo kuna vijana wa kazi," alisema Tadayo.

Aliwataka vijana kuungana na kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kuhakikisha jimbo hilo linarudi CCM ifikapo mwaka 2020 katika uchaguzi mkuu.

Alisema kuwa, jimbo hilo linachangamoto mbalimbali ambazo zilistahili kutatuliwa na mbunge wa jimbo, lakini katika hali ya kushangaza ameshindwa kufanya hivyo na kudai kuwa angekuwa anatokaa CCM angemwita kujibu tuhuma hizo.

"Mbunge wa Jimbo hili anatoka chama cha upinzani (Chadema), angekuwa ni mbunge wa CCM ningemuita sasa hivi hapa mbele yenu aeleze ni kwa nini anashindwa kuwatumikia na kuwatatulia matatizo yenu, lakini kwa hapa sina uwezo," alisema Tadayo.

Aidha, aliwataka vijana hao kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika chaguzi za serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu mwakani ili kuhakikisha maendeleo yanasonga mbele.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agnes Hokororo, alisema kuwa wilaya hiyo imekuwa ikiandamwa na kashfa za vijana wake kutekwa na ulevi wa kupindukia madai ambayo ameyakanusha baada ya kushuhudia wanavyochapa kazi.

Hokororo alisema, vijana hao wamekuwa wakijituma kila kukicha kuhakikisha maendeleo ya Rombo yanasonga mbele na kuongeza kuwa kwa sasa vijana hao wameshaanza kujipanga ili kuhakikisha jimbo hilo linarejea CCM ikiwa ni dhamira ya kumuunga mkono Rais Magufuli.

Akizungumzia suala la ulevi, Mwenyekiti huyo wa Ulinzi na Usalama wa wilaya alisema kuwa, wamekuwa wakiendelea kudhibiti ulevi na kuwa mapambano hayo ni endelevu.




Mmoja ya watalii kutoka Kampuni ya KiliTwende Tours, akiwa amejilaza katika kibao cha Lava Tower Camp kutokana na uchovu wakati wa safari yake ya kupanda Mlima Kilimanjaro hadi kilele cha juu kabisa cha Uhuru Peak chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari. **PICHA:JAMES LANKA**

# Kinamama Kia walia unyanyasaji

**Na Mary Mosha,** HAI

KINAMAMA Kata ya Kia, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia Jeshi la Polisi la kituo kidogo cha Kia kwa madai ya kuwatesa watoto wanapokuwa malishoni kwa kufyatua risasi hewani katika makazi yao huku wakiwatolea maneno ya udhalilishaji.

Wakiongea mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, Anastasia Moleli, alisema kuwa wapo baadhi ya askari wamekuwa wakiwatolea lugha chafu watoto wao bila sababu za msingi wakati wanapokuwa malishoni.

Raheli Leiza, alisema mbali na kuwatolea lugha za udhalilishaji, pia wamekuwa wakiwapa adhabu za kuwatumbukiza kwenye madimbwi ya matope nyakati za mvua na kuwaanika kwenye jua kali nyakati za ukame hali inayowasononesha wazazi.

"Askari hawa wa Kia wamekuwa wakiwatumbukiza watoto wetu kwenye madimbi ya matope wakati wa masika, na wakati wa kiangazi kuwatoa nguo na kuwaanika kwenye jua kali na vumbi, hii sio haki tunamuomba mkuu wa mkoa kuingilia kati ili tuweze kujua hatima yetu," alidai mama huyo na kuongeza:

"Hawaishii hapo tu, wamekuwa wakiwakimbiza hadi kwenye maboma yetu na kurusha risasa juu hali ambayo ni hatari kwa wazee, wanawake wajawazito na wenye shinikizo la damu...pia watoto hao wanapofika nyumbani tunalazimika kuwakimbiza hospitali na kutumia gharama kubwa katika kuwatibu," alidai.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sanya, Satition Kera Komea, alikiri kupokea taarifa hizo za askari kuvamia eneo na kupiga risasi hewani kwenye makazi ya watu kwa kile kilichodaiwa kuwafukuza watoto waliokuwa wakilisha mifugo.

"Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwaonya hawa polisi maana sio mara ya kwanza kuwanyanyasa watoto na kinamama ... tumevumilia kwa heshima ya serikali yetu, lakini ipo siku tutachoka kuvumilia na kunaweza kutokea machafuko," alionya.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kia, Yohana Leiza, alisema tatizo hilo limekuwa likijirudia mara kwa mara bila sababu za msingi huku kinamama na watoto wakiendelea kuteseka.

"Mkuu wa Mkoa, Polisi wa Kia wamefanya kama huu ndio mtaji wao kukamata mifugo yetu na kuipeleka mahabusu bila kuipa chakula wala maji huku wakisubiria kulipwa kiasi cha Sh. 200,000 kwa kuwa wanadai mifugo hiyo imekuwa ikiingia kwenye eneo lililokatazwa," alidai.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema serikali imekuja kusimamia haki na amani kwa pande zote mbili na sio kuruhusu eneo hilo kuwa uwanja wa mapambano.

Alikemea tabia ya askari kukimbiza watoto kwa kutumia magari pale wanapokuwa malishoni na kumuagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimamanjaro, kuwachukulia askari hao hatua wakiwamo wanaodaiwa kurusha risasi kwenye makazi ya watu.

## Diwani, Katibu mwenezi waihama Chadema

**Na Paul William,** MOSHI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeendelea kupukutika baada ya aliyekuwa Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi na Katibu Mwenezi wa chama hicho Jimbo la Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro, Deogratius Mushi, kukihama chama hicho na kutimkia CCM.

Kuhama kwa diwani huyo kunafanya idadi ya madiwani waliojiuzuru na kutoka Chadema kurudi CCM kufikia 18 katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mushi aliwahi kugombea ubunge katika Jimbo la Kawe, jijini Dar es Salaam, mwaka 2005, na badaye alifanikiwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho.

Alitangaza rasmi kuhamia CCM juzi na kukabidhi kadi ya Chadema kwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, katika ofisi za chama hicho mkoa.

Boisafi alisema kuwa, kazi ya Chama cha Mapinduzi ni kushika dola na kuwatumikia wananchi kwa kutatua kero mbalimbali zinazowakabili na mwaka 2015 wapo baadhi ya wana-CCM waliamua kuhamia upinzani, lakini baada ya kufika kuona yale waliyotegemea hayafanyiki, wameanza kurudi.

"Chama chochote chenye malengo ya kushika dola ni lazima kiwe na mtaji wa wanachama hivyo sisi kama chama tawala tunaendelea kuwapokea wanachama wetu waliokuwa wamepotea na sasa wanataka kurudi nyumbani," alisema Boisafi.

Alisema kuwa, wanachama wote wanaorejea sasa, chama kitawatumia kuongeza nguvu katika chaguzi mbali mbali zikiwamo za serikali za mitaa ili kuhakikisha kuwa upinzani unatoweka katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa upande wake, Mushi alisema ameamua mwenyewe kwa hiari yake kujiuzulu udiwani pamoja na nafasi zote ndani ya Chadema na kutimkia CCM kutokana na chama hicho kuendesha kwa lengo la maslahi ya watu wachache.

"Chadema ni kundi dogo la watu waliojilimbikizia madaraka na hawawezi kuipeleka mbele taifa hili na kuwaletea wananchi maendeleo kamwe na ni kutokana na ulafi wa madaraka na kutaka kujinufaisha baadhi ya watu na familia zao," alisema Mushi. Alisema kuwa, kitendo cha yeye kutoka Chadema na kuhamia CCM hataachana na siasa na kutumia nafasi hiyo kukiomba CCM wakiona inafaa wampe ridhaa ya kupeperusha bendera yake katika uchaguzi utakaofanyika katika kata hiyo.

"Nimechoka kuvaa manguo ya migambo wakati hata sijawahi kupitia mgambo wenyewe halafu unakuta kiongozi anakwambia komaa kamanda unajiuliza tangu lini nimekuwa kamanda, nimeamua kurudi kuvaa nguo za heshima za CCM," alisema Mushi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi, Kastori Msigala, alikiri kupokea barua ya kujiuzulu kwa diwani huyo na kuachia nafasi zote ndani ya Chadema na kujiunga na CCM na alisema kuwa kwa sasa ameshatoa taarifa Wizara ya Tamisemi ili hatua nyingine ziweze kufuatwa.

# Nipashe Spotika



NYOTA WA4 WALIOSTAHILI KUWAMO KIKOSI CHA PFA UK.14



## ISIKUPITE

USHINDI wa mabao 2-0 Liverpool iliyoupata dhidi ya Cardiff City wiki iliyopita, umemfanya kipa Alisson kumaliza mechi bila kuruhusu bao [clean sheets] katika michezo 19 msimu huu. Na kwa idadi hiyo Alisson, 26, anaipiku rekodi ya mechi 18 bila kuruhusu bao iliyokuwa ikishikiliwa na David de Gea katika kipindi cha muongo mmoja. Kipa anayeshikilia rekodi ya 'clean sheets' ni Petr Cech, ambaye aliiweka msimu wa 2004-05 baada ya kutoruhusu bao katika mechi 24 msimu huo.

# LA UBINGWA...

Lionel Messi akifunga bao pekee lililoiwezesha Barcelona kushinda 1-0 dhidi ya Levante na kutangazwa mabingwa wa La Liga rasmi juzi. **HABARI UK. 28**

SOKA



# NYOTA WA4 WALIOSTAHILI KUWAMO KIKOSI CHA PFA

**LONDON,** England

SI jambo la kushangaza kwamba wachezaji 10 kati ya 11 kwenye timu ya mwaka ya PFA wanatoka ama Manchester City au Liverpool, kwani ndio wametawala ligi msimu huu.

**Hata hivyo, kumuona Paul Pogba halikuwa pia jambo la kushangaza. Lakini pia katika orodha hiyo kuna majina ya wachezaji ambao hawapo.**

Hapa tunawaangalia wachezaji wanne ambao walistahili kuwapo kwenye kikosi hicho ambao walionekana kuwa na msimu mzuri zaidi.

**4. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL)**

Akiwa amefunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho saba kwenye Ligi Kuu ya England, kunamfanya kuwa mmoja wa wachezaji walioonyesha kiwango cha juu zaidi msimu huu.

Kuondolewa kwa Salah katika kikosi hicho kunaonyesha kwamba tayari Liverpool wametoa wachezaji wanne huku Sadio Mane akiwamo. Lakini bado kuna swali kubwa kwamba kwa nini Salah hajajumuishwa.

Kwa mfano, raia huyo wa Misri amecheza dakika 200 kuliko Mane raia wa Senegal, huku pia akiwa amepiga mashuti 40 kuliko Mane aliyepiga mashuti 19.

Lakini kwa mshangao wa wengi, Salah hajajumuishwa kwenye kikosi hicho, huko Mane akiwa kwenye orodha hiyo.

**3. N'GOLO KANTE (CHELSEA)**

Kama unafikiria kazi ya N'Golo Kante ni kukimbia tu uwanjani unakosea, kwani kazi anayoifanya ni kubwa mno katika kuhakikisha anaichezesha timu yote.

Baada yakushinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa kipindi cha majira ya joto mwaka jana, akitoka kushinda mara mbili taji la Ligi Kuu ya England na mchezaji bora wa msimu, kumeibua maswali kwa nini Kante ameachwa. Nini cha zaida ambacho alitakiwa kukifanya? Jibu ni kwamba kufunga mabao mengi zaidi.

Huku Jorginho alitarajiwa kuwa mchezaji wa kiungo atakayemsaidia zaidi Sarri, lakini ni ukweli kwamba Kante ndiye alikuwa na wakati mzuri zaidi. Ameichezea timu hiyo kwenye safu ya kiungo kwa kuiunganisha na ya ushambuliaji na ulinzi na pia kuwa kama kiungo mkabaji. Ukiacha kutaja mabao yake dhidi ya Manchester City na Tottenham, bado alipaswa kuwapo katika kikosi hicho cha mwaka.

**2. SON HEUNG-MIN (TOTTENHAM)**

Mmoja wa wachezaji muhimu kwa Tottenham msimu huu hakuwa Harry Kane au kiungo Christian Eriksen. Pia si Dele Alli wala Lucas Moura. Huyu ni Son Heung-Min.

Ulazima wa kwenda kulitumikia kwanza jeshi nchini kwake Korea Kusini kulisababisha kukosa mwezi wote wa kwanza wa Ligi Kuu. Lakini Son amelipa fadhila kwa kiwango alichokionyesha msimu huu. Akiwa amefunga mabao 12 na pasi za mwisho saba hadi sasa, amekuwa ni mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi cha Spurs msimu huu baada ya kuumia kwa Kane.

Alikuwa ndiye nguzo wakati wakitoa Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini kwa mshangao wa wengi hakuwapo kwenye kikosi cha mwaka cha EPL msimu huu.

**1. EDEN HAZARD (CHELSEA)**

Wengi walishangaa zaidi kutoliona jina la mchezaji huyu wa Chelsea, Eden Hazard.


Kulikuwa na sababu nyingi za kumjumuisha Hazard katika kikosi cha mwaka kutokana na ukweli kwamba, amekuwa na mchango mkubwa kwa 'Blues' hao msimu huu.

Chelsea baada ya kuwa na safu mbovu ya ushambuliaji na kuamua kumuuza Morata, ilimchukua kwa mkopo Higuain ambaye ameshindwa kabisa kuwa suluhisho la mabao kwa kikosi hicho.

Lakini Hazard licha ya yeye kucheza kama kiungo mshambuliaji, ndiye amekuwa kwenye orodha ya wafungaji mabao wa Chelsea na kuisaidia kufika hapo ilipo.

Akiwa na mabao 16 kwa jina lake, yeye alipaswa kuwapo kwenye kikosi cha mwaka kutokana na mchango wake mkubwa kwa kikosi hicho msimu huu.

**JE, WAJUA?**



NI Jose Mourinho pekee amemfunga kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino mara nyingi zaidi (mara 5) kwenye Ligi Kuu England kuliko Manuel Pellegrini (mara 4, sawa na Pep Guardiola).

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA

# Pochettino aiota Ajax

MAURICIO Pochettino amekionya kikosi chake kusahau kipigo cha Jumamosi cha bao 1-0 kutoka kwa West Ham United kwenye Ligi Kuu ya England, wakati wakiivaa Ajax kesho Jumanne kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Spurs ilikumbana na kipigo cha kushitukiza kwenye mchezo huo na hivyo kujiweka kwenye hatari ya kupokonywa nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na waandishi mara baada ya mchezo huo, Pochettino alisema kwa sasa wachezaji wake wanapaswa kusahau kipigo walichokipata kutoka kwa West Ham na kuwataka kuelekeza akili yao kwenye mchezo dhidi ya Ajax.

"Tunatakiwa kusahau kuhusu hilo, twende mbele na kufikiria mchezo wa Jumanne," alisema Pochettino.

"Ni ngumu kuandaa nusu fainali dhidi ya timu ngumu kama Ajax, tunatakiwa kujipanga na kusahau yaliyopita."

Pochettino, ambaye alifanya mabadiliko kutoka kwenye mchezo wa katikati ya wiki wa ushindi dhidi ya Brighton, alikanusha taarifa kwamba Moussa Sissoko na Harry wako fiti.

"Bado hawajapona vizuri na la muhimu ni mchezo wetu unaokuja tu, hivyo mengine yatazungumza baadaye."






Beki wa KMC FC, Ismaili Gambo (chini), akijaribu kumdhibiti John Bocco wakati wa mechi ya Ligi Kuu Bara, iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba juzi na Simba kushinda 2-1.

# OKWI, BOCCO MBELEKO SIMBA KANDA YA ZIWA

**Na Somoe Ng'itu,** MUSOMA

ILIKUWA ni dakika 360 za jasho na damu kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam kwenye mikoa minne ya Kanda ya Ziwa wakati wakivuna pointi tisa.

**Mikoa hiyo ni Kagera, Mwanza na Mara ambapo Simba ilicheza mechi hizo kwa kutumia siku tano, ikiwa ni muda ambao si rafiki sana kwa afya za wachezaji na hazifiki saa 72 kutoka mechi moja hadi nyingine kama kanuni za ligi hiyo zinavyoelekeza.**

Katika dakika hizo walizocheza, Simba iliyokuwa inakabiliwa na michezo minne ya ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kila mwaka ambayo ilipewa jina maarufu la "viporo" ilivuna pointi tisa kati ya 12 ambazo ilikuwa inazihitaji.

Mechi hizo ilikuwa ni dhidi ya Kagera Sugar ambayo ilipoteza kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1, halafu ikatua Mwanza na kupata ushindi wa mabao 2-0 na ikamaliza na mchezo wake wa pili kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo kwa kuifunga KMC FC 2-1.

Baada ya mchezo huo dhidi ya KMC, vigogo hao wa Dar es Salaam walisafiri kuja mjini hapa kwa kucheza na Biashara United iliyoko chini ya beki wake wa zamani, Amri Said na kupata pointi nyingine tatu kutokana na kuwafunga wenyeji hao mabao 2-0.

Hata hivyo, haikuwa kazi rahisi kwa Wekundu wa Msimbazi kupata ushindi katika mechi tatu kutokana na kukutana na timu zilizokuwa katika janga la kushuka daraja (Kagera Sugar, Alliance FC na Biashara United) na moja ambayo ni KMC FC iliyohitaji kujiimarisha zaidi katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 20.

Ushindi wa mabao 2-1 walioupata Kagera Sugar uliwasaidia kuwatoa katika nafasi ya 17 hadi ya 13 katika msimamo na kuwafanya waanze kujinasua na janga la kushuka daraja ambalo mpaka sasa bado hazijajulikana timu halisi zitakazopitiwa na panga hilo.

### OKWI, BOCCO WANG'ARA

Katika mechi nne walizocheza katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Simba ilifanikiwa kufunga mabao saba.

Wafungaji wa mabao hayo waliyowapa pointi tisa na kufikisha jumla ya pointi 69 walikuwa ni Emmanuel Okwi aliyecheka na nyavu mara tatu na nahodha, John Bocco aliyefunga idadi kama hiyo.

Bao lingine lilifungwa na kiungo Mnyarwanda, Haruna Niyonzima ambaye alikuwa anafungua akaunti yake ya mabao msimu huu unaoelekea ukingoni, kwa kufunga bao moja kwenye ushindi wa 2-0 dhidi ya Alliance FC.

Hata hivyo, Simba katika mechi hizo nne, iliruhusu nyavu zake kutingishwa mara mbili, langoni akiwa amesimama, kipa Aishi Manula huku Deogratius Munishi "Dida" akidaka mchezo mmoja na alifanikiwa kulinda vyavu zake zisitingishwe.

Mechi zote zilikuwa na ushindani kutokana na kila upande kuhitaji kutimiza malengo yake katika dakika hizi licha ya kuzungukwa na changamoto za hapa na pale.

### AUSSEMS- HAIKUWA KAZI RAHISI

Kucheza mechi kila baada ya siku moja haikuwa kazi rahisi kwa mabingwa hao watetezi ambao msimu huu walifika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya kutolewa kwa jumla ya mabao 4-1 na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kocha wa Simba, Patrick Aussems, alisema kuwa alilazimika kupangua kikosi chake cha kwanza ili kuweka mipango ya kupata ushindi huku wakipambana na ratiba ngumu iliyokuwa inawakabili.

Aussems alisema kuwa alilazimika kuchezesha wachezaji kwa mzunguko na uamuzi huo umemsaidia kupata matokeo chanya katika mechi tatu kati ya nne zilizokuwa zinawakabili katika kanda hiyo.

"Mfumo huu wa kubadilisha kikosi ni kwa ajili ya kuwafanya wachezaji wapate nguvu na kupumzika, kucheza siku moja na siku inayofuata unasafiri ni changamoto kubwa, kuna mechi wamecheza vizuri na kushinda, na nyingine tumepata pointi tatu na kushinda tu, lakini hatukucheza vizuri," alisema kocha huyo.

### ...YATETEMA MUSOMA

Kikosi cha Simba kilipata mapokezi makubwa zaidi katika mji wa Musoma huku ikifuatiwa na Bukoba.

Mashabiki wa timu hiyo mjini hapa, walijitokeza kuipokea timu hiyo kuanzia eneo la Makutano wakiwa katika msafara wa magari madogo na pikipiki.

Mwenyekiti wa Tawi la TAS Musoma, Ramadhani Mahano, aliliambia gazeti hili kuwa wanalishukuru Jeshi la Polisi kwa kusaidia ulinzi wakati wa mapokezi ya timu yao.

"Hatukuwa tumepeleka maombi yoyote kwa Jeshi la Polisi, lakini kwa hali ilivyokuwa, walilazimika kuja kuongoza magari na kutoa ulinzi wa kiwango cha juu, kweli hii timu ni mabingwa na wa kimataifa, tunasema asante kwa mashabiki wote wa Simba hapa Musoma," alisema mwenyekiti huyo.

Katika kuonyesha mashabiki hao walijiandaa vema kwenda kuishangilia timu yao, serikali ya mkoa kupitia kiongozi wake mkuu, Adam Malima, ilielekeza milango ya Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume ifunguliwe mapema zaidi.

Awali milango hiyo ilipangwa kufunguliwa kuanzia saa 4:00 asubuhi, lakini ilibidi mageti yafunguliwe kuanzia saa 2:00 asubuhi ili kuruhusu mashabiki waliofika uwanjani hapo na wana tiketi mikononi waweze kuingia.

## Extra Time

# NANI NI NANI KUELEKEA MWISHO WA MSIMU EPL



VAN DJIK

AGUERO

**LONDON,** England

MSIMU wa sasa wa Ligi Kuu ya England umekuwa mmoja kati ya unaoburudisha zaidi katika siku za hivi karibu.

**Manchester City na Liverpool zinapigana vikumbo kuwania taji hilo, huku Tottenham Hotspur, Arsenal, Chelsea, na Manchester United zikijaribu kuipigania nafasi nne za juu.**

Na wakati zikiwa zimebakia wiki tatu ligi hiyo kufikia tamati, bado hakuna mwenye uhakika. Hapa tunaangalia siku za mwisho za ligi hiyo zinavyoweza kuamua bingwa na nne-bora...

### VITA NI VITA TAJI LA EPL

Manchester City na Liverpool hazijawahi kufikia kwenye mbio moja za kuwania ubingwa wa EPL. Lakini msimu huu ndio mara yao ya kwanza zikipigania kwa pamoja taji hilo. Ukweli ni kwamba timu moja inaweza kufikisha pointi 97 na bado inakuwa katika nafasi ya pili na hapo ndipo Liverpool inapoweza kujikuta.

Manchester City ilimaliza msimu uliopita na ndio inaonekana wanaweza kufanya hivyo msimu huu. Lakini Liverpool walikuwa na moja ya vikosi bora zaidi kwenye Ligi Kuu. Ukweli ni kwamba timu hizo mbili za juu zinaongoza kwa tofauti ya pointi 21 na 19 dhidi ya timu zinazowafuata, hiyo ikiwa ni kabla ya mechi za jana.

Na pia inaonyesha kwamba kama si Liverpool, Man City wanaweza kurudia mafanikio yake ya kihistoria ya msimu uliopita.

Sasa mechi zilizobaki kumalizika kwa ligi hiyo kwa timu hizo mbili, Liverpool inaonekana kuwa na mechi rahisi zaidi. Ijumaa walicheza na Huddersfield Town nyumbani, wataikabili Newcastle United ugenini na Wolverhampton Wanderers nyumbani kwenye mchezo wa mwisho.

Manchester City wao jana walikuwa na mechi dhidi ya Burnley ugenini, kisha watacheza dhidi ya Leicester City nyumbani na kumaliza msimu na Brighton & Hove Albion ugenini.

Chochote kitakachotokea ni kwamba yeyote kati yao anaweza kulitwaa taji hilo msimu huu. Nani atalibeba?

### MBIO ZA NNE BORA

Mbio za nne bora zipo kwa timu nne msimu huu. Tottenham Hotspurs, Arsenal, Chelsea, na Manchester United zote zinaangalia nafasi ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ukiziangalia timu hizi, na inaonekana wazi kwamba hakuna hata moja ambayo ipo tayari kuiachia nafasi hiyo.

Tottenham Hotspurs imekuwa na msimu mzuri zaidi, ikiwa kwenye nafasi ya tatu. Haikufanya usajili mkubwa wakati wa kipindi cha majira ya joto huku karibu msimu mzima ikitumia Uwanja wa Wembley kama ndio dimba lake la nyumbani.

Katika mechi zake za mwisho za ligi hiyo wana nafasi ya kubakia kwenye nafasi hiyo. Tottenham imebakiwa na mechi dhidi ya Bournemouth ugenini na Everton nyumbani.

Arsenal imekuwa inapanda na kushuka msimu huu. Walianza msimu huu kwa kupoteza dhidi ya Manchester City na Chelsea. Halafu wakacheza mechi nyingi bila kufungwa. Baada ya hapo 'Washika Bunduki' hao wamekuwa kwenye kiwango kisichoridhisha. Baada ya mechi ya jana dhidi ya Leicester ugenini, Arsenal itamaliza dhidi ya Brighton nyumbani na Burnley ugenini.

Kati ya timu nne zinazowania nafasi hizo mbili, Chelsea walikaribia kwenye nafasi hiyo. Wakati huu ikiwa kwenye adhabu ya kutosajili, inaweza kuipigania nafasi hiyo. Kama ilivyo kwa Arsenal, Chelsea haijawa kwenye kiwango cha kuridhisha. Kwenye mechi zake za mwisho baada ya kuivaa Manchester United ugenini jana, itacheza sasa dhidi ya Watford nyumbani na Leicester City ugenini.

Chini ya Jose Mourinho, Manchester United ilianza msimu kwa nguvu na baadaye kusuasua. Kisha akafukuzwa Desemba na akapewa Ole Gunnar Solskjaer ambaye naye alianza vizuri, lakini sasa mambo yamekuwa tofauti.

Manchester United inakabiliwa na mechi ngumu za mwisho, kwani baada ya kuialika Chelsea jana, itamliza mbili za mwisho dhidi ya Huddersfield ugenini na kisha Cardiff City nyumbani.

### NAFASI NYINGINE

Nafasi ya saba kwenye Ligi Kuu ina faida na hasara. Faida ya atakayemaliza nafasi ya saba anaweza kufuzu kucheza Ligi ya Europa.

Watford, Everton, Leicester City na Wolverhampton Wanderers ndizo zilizopo kwenye mbio moja ya kuwania kumaliza nafasi ya saba.

Everton kwenye mechi za mwisho itacheza na Burnley nyumbani na Tottenham ugenini. Watford itacheza dhidi ya Chelsea ugenini na West Ham nyumbani. Huku Leicester City itamaliza msimu kwa mechi dhidi ya Manchester City ugenini na Chelsea nyumbani.

Timu iliyopanda daraja Wolverhampton Wanderers itacheza na Fulham nyumbani na Liverpool ugenini. Je, nani atafuzu kucheza Ligi ya Europa?

### KUSHUKA DARAJA

Tayari Huddersfield na Fulham zimeshashuka daraja na msimu ujao zitacheza kwenye Ligi ya Championship. Cardiff inapigania kubakia kweye Ligi Kuu. Timu nyingine kama Brighton na Southampton nazo zipo kwenye hatari ya kushuka daraja.

Cardiff itamaliza msimu kwa mechi dhidi ya Crystal Palace nyumbani na Manchester United ugenini. Brighton itacheza na Arsenal ugenini na Manchester City nyumbani, wakati Southampton itacheza dhidi ya West Ham ugenini na Huddersfield nyumbani.

Nani atatwaa ubingwa, atafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, atakata tiketi ya kucheza Europa na atayeungana na Huddersfield na Fulham kushuka daraja? Ni suala tu la kusubiri na kuona.

## Nukuu

"Kumekuwa na mengi yanazungumzwa kuhusu Virgil van Dijk. Nilijua atakuwa na kura nyingi, hivyo nikatazama mtu fulani niliyedhani atakuwa karibu yake katika timu ya taifa, jinsi anavyoiweka kazi yake, maadili ya kazi, jinsi anavyojiangalia. Mara zote yupo pale, zaidi akitokea katika kuuguza majeraha, kama mtaalamu nilimtazama yeye [Harry Kane] na hiyo ndiyo sababu ya kumpigia kura," **Raheem Sterling akitoa sababu ya kumpa kura Kane na kumtosa Van Djik katika kinyang'anyiro cha tuzo ya PFA.**




"Wangeweza kuwa wanne, watano, sita au saba zaidi [kwenye kikosi bora cha msimu cha PFA], walicheza vizuri zaidi kwa msimu mzima. Kwa upande wangu timu yangu ni bora zaidi kwa msimu," **Jurgen Klopp akieleza baadaya wachezaji wanne tu wa Liverpool, Andrew Robertson, Trent-Alexander Arnold, Virgil van Dijk na Sadio Mane kujumuishwa katika kikosi bora cha msimu cha PFA**



"Kiukweli Simba haina mpango na [Jacques] Tuyisenge, tunahitaji kuwa na mshambuliaji ambaye anawazidi kwa mbali [John] Bocco, Okwi [Emmanuel], [Meddie] Kagere, hawa wote ni wachezaji ambao wanacheza kwenye boksi, sasa anayetakiwa ni mwenye uwezo wa kufanya vitu vyote wakiwa nje ya boksi ili tufike tunakokuhitaji," **Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori.**





# KWA NINI AUSSEMS NI HAKI KUBAKI SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MKATABA wa Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, unamalizika mara tu baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kufikia tamati Mei mwaka huu ambapo klabu hiyo itakuwa na uamuzi mmoja wa kusuka au kunyoa.

**Ni kuachana naye na kutafuta kocha mwingine, au kumpa mkataba mpya ili aendeleze pale alipofikia, taarifa zisizo rasmi zinadai kuwa ndani ya Simba kumekuwa na mgawanyiko wa Wajumbe wa Bodi, wengine wakitaka aendelee na kazi yake kwa sababu ameifikisha timu pazuri, hasa kwenye michuano ya kimataifa, lakini wengine wanapinga na kutaka atafutwe kocha mwingine kwani pamoja na mazuri yake, lakini amekuwa na mapungufu hasa timu inapokwenda kucheza ugenini.**

Hata hivyo, taarifa zingine zinadai kuwa kuna asilimia kubwa kwa kocha huyo kuongezwa mkataba kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kuwa na mahusiano mazuri na wachezaji na tayari ameshawazoea, hivyo kumleta kocha mwingine kunaweza tena kuifanya timu ianze upya.

Mwandishi wa makala haya anakulea sababu ambazo zinamfanya kocha huyo kuwa lulu na bado kutakiwa kuendelea kubaki na klabu hiyo kwa mara nyingine tena.

**1. KULETA MSHIKAMANO KWA WACHEZAJI**

Kwa muda mrefu sasa hakujasikika minong'ono au tetesi juu ya kuwa na mgomo baridi, mgogoro au kutokuelewana kwa wachezaji wenyewe kwa wenyewe au na kocha ndani ya timu hiyo.

Kwa klabu kama ya Simba hilo limekuwa ni jambo adimu, kwani mara kwa mara imekuwa moja ya timu ambayo wachezaji wake wamekuwa wakizua migomo baridi na manung'uniko ya hapa na pale.

Mgogoro wa mwisho kwenye kikosi ulikuwa pake kocha huyo alipokuwa na msaidizi Masud Djuma. Ilidaiwa na kuthibitishwa na uongozi wa Simba kuwa kulikuwa na kutoelewana baina ya makocha hao wawili.

Duru zikasema kuwa Djuma alikuwa ameshatengeneza kikosi cha wachezaji wa kumhujumu Mbelgiji ili timu ifanye vibaya kabla ya kufukuzwa na timu akabidhiwe yeye.

Lakini tangu alipoondoka Djuma, timu imetulia. Wachezaji wametulia na wamekuwa wamoja kama familia moja na kocha huyo pamoja na kwamba ni kosa na yuko kazini, lakini pia amekuwa akiwalea kama mzazi, kitu ambacho kimefanya wachezaji kumpenda na kumkubali.

**2. KUMPA NAFASI KILA MCHEZAJI**

Moja ya matatizo yanayofanya kuwa na migogoro au mgomo baridi wa wachezaji ndani ya timu ni upendeleo kwa baadhi ya wachezaji.

Kuna baadhi ya wachezaji wanapata nafasi ya kucheza, lakini wengine hawapati, huku ikionekana ambao hawapati wana uwezo kuliko baadhi ya wachezaji wanaopangwa. Hili halipo kwa Aussems. Amekuwa akiwachezesha karibuni wachezaji wote wa Simba kwa nyakati tofauti.

Pamoja na kwamba amekuwa akizingatia uwezo wa wachezaji, lakini hata wale ambao wanaotajwa kuwa ni wachezaji wa benchi wamekuwa wakipata nafasi ya kuonyesha uwezo wao kwenye baadhi ya mechi.

Chini ya kocha huyo, ni mchezaji mwenyewe ndiye atakayekuwa anajiangusha kwa kutoonyesha kiwango, lakini amejitahidi sana kumpa nafasi kila mmoja kuthibitisha uwezo wake wa kuisaidia timu.

Mfano Haruna Niyonzima ambaye dakika chache tu kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita, zimebadilisha kabisa mtazamo wa wengi kuwa amekwisha. Na hili la kumpa nafasi kila mchezaji limempa heshima na kukubalika mno mbele ya wachezaji wote wa Simba, hivyo sidhani kama viongozi watataka kuvuruga amani hiyo iliyopo.

**3. KUTOFOKEA OVYO WACHEZAJI UWANJANI**

Kocha huyo hana tabia ya kuwafokea ovyo wachezaji wake uwanjani wanapofanya vibaya au kukosea. Hii ni tofauti na makocha wengi ambao wamekuwa wakiwapigia kelele na kuwafokea wachezaji uwanjani, kiasi wakati mwingine kuwachanganya.

Na hata kama kuna makosa, amekuwa akiwaita na kuwaambia kwa taratibu na hii imemjengea heshima kwa wachezaji ambao wanaonekana kuheshimu mawazo yake.

**4. KUIFIKISHA SIMBA ROBO FAINALI AFRIKA**

Heshima kubwa aliyonayo Aussems kwa sasa ni kuifikisha Simba hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kitu ambacho hakikufanywa na kocha yoyote wa klabu hiyo kwa miaka 24 iliyopita.

Mara ya mwisho kwa Simba kufikia hatua hiyo ilikuwa ni mwaka 1994 na kutolewa na Nkana Red Devils ya Zambia ilipofungwa mabao 3-0 nchini Zambia, kabla ya kushinda mabao 2-0 nyumbani, matokeo ambayo yalishindwa kuivusha hatua ya nusu fainali kwa jumla ya mabao 3-2.

Kwa kuwashangaza mashabiki wa soka Afrika kwa kufikia hatua hiyo, Aussems alikuwa na wachezaji wa kiwango cha kawaida sana Afrika.

Ameonekana kuwa ni kocha bora katika ufundishaji, lakini pia ni mzoefu kwenye michuano ya kimataifa, hasa Ligi ya Mabingwa akiwa na klabu mbalimbali kubwa alizowahi kufundisha, ikiwamo Wydad Casablanca ya Morocco. Kocha huyo aliletwa Simba wakati tayari ikiwa imefanya usajili, hivyo matumaini ya wengi ni kufanya vizuri zaidi ya hapo kama atapendekeza mwenyewe wachezaji anaowahitaji, huku viongozi wa Simba wakilenga kusajili wachezaji wa viwango vya juu barani Afrika.

**5. HANA MBWEMBWE**

Tofauti na baadhi ya makocha wengine wa Simba waliopita, Aussems si muongeaji sana na badala yake anaongoza zaidi kwa vitendo kuliko mdomoni.

Tofauti na mwili wake jinsi ulivyo, kocha huyo amekuwa kinyume kabisa na muonekano wake, hata uwanjani amekuwa hana mbwembwe nyingi, kitu ambacho baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba awali waliona kama mapungufu makubwa kwake, kuliko Masudi aliyekuwa na mbwembwe nyingi.

Kutoongea vitu vingi visivyomhusu, badala yake kuongelea kazi yake iliyomleta, pamoja na kutokuwa na mambo mengi hata nje ya uwanja, kumemjengea heshima kubwa kwa Wanasimba na kuonekana kuwa ana hadhi ya kuwa kocha wa klabu kubwa kama Simba.

**NAJUA WAJUA**



Tottenham imepoteza mechi 17 katika mashindano yote msimu huu, idadi ambayo ni kubwa zaidi kwao tangu msimu wa 2008-09 ilipopoteza mechi 19.

## SOKA



# SABABU 3 MAN UNITED KUANGUKA MSIMU HUU

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United mara zote si tu imekuwa ni klabu kubwa England, lakini pia kwa Ulaya yote. Wengine wamekuwa wakiitaja kama ndio klabu bora zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya soka la Uingereza. Na sababu kubwa ni mtu mmoja naye ni Sir Alex Ferguson.

**Tangu Ferguson alipostaafu kutoka kuwa bosi wa United, klabu hiyo imepitiwa na makocha kadhaa kuiongoza kwenye zama mpya. Ilianzia kwa David Moyes, baadaye Louis van Gaal, halafu Jose Mourinho, na kwa sasa inaongozwa na kocha Ole Gunnar Solskjaer.**

Lakini kati ya hao hakuna kocha ambaye amejaribu kufikia mafanikio ya Sir Alex, huku Mourinho akijipa mafanikio kwa kubeba taji la Ligi ya Europa mwaka 2017.

Msimu huu mambo yameonekana kuendelea kuwa ovyo kama ilivyokuwa kwa kocha Mourinho na Ole anaelekea kushindwa kuiongoza kwenye kuelekea mafanikio. Lakini kiukweli kabisa kiwango cha sasa cha United kimekuwa ni cha kuhuzunisha.

Hapa tunaangalia sababu tatu ambazo zimeifanya klabu hiyo kuanguka msimu huu na kuwa kwenye kiwango kibovu kabisa.

**3. KUKOSEKANA SAFU IMARA YA ULINZI**

Alex Ferguson aliwahi kunukuliwa akisema, "safu ya ushambuliaji inakufanya ushinde mechi, lakini safu ya ulinzi inakufanya ushinde mataji."

Manchester United tatizo lake kubwa zaidi ni kwenye safu ya ulinzi. Safu ya ulinzi ya wachezaji wanne imekuwa mbovu zaidi kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita au pengine kwenye historia ya klabu hiyo.

United ilishuhudia zama za Vidic na Ferdinand wakishinda mataji kwa kuwa kwenye kiwango kisichoshuka, lakini sasa safu ya ulinzi ya klabu hiyo imekuwa mbovu zaidi na mashabiki wamekuwa wakilipigia kelele hilo.

Ingawa Victor Lindelof amekuwa kwenye kiwango kizuri zaidi msimu huu ikilinganishwa na wachezaji wengine, lakini tatizo lake moja ni kwamba hakuzaliwa kuwa kiongozi kama alivyokuwa Vidic. Ashley Young amekuwa kwenye kiwango kibovu. Smalling na Jones ni mabeki wazuri lakini hawastahili kuichezea klabu kama Manchester United. Na kipaji cha Luke Shaw kimekumbwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Kwa sasa Manchester United inahitaji beki aina ya Van Dijk ambaye alisajiliwa na Liverpool na kumfanya kuwa mmoja wa mabeki bora barani Ulaya kwa sasa. United pengine inamhitaji mtu kama Van Dijk kwa sasa.

**2. KUKOSEKANA KWA UONGOZI BORA**

United wamekuwa wakicheza kwa staili ya tofauti dimbani, badala ya kuwa na mpango wa ushindi katika mchezo. Mara zote wakati Solskjaer akiwa anazungumza na waandishi wa habari amekuwa akijaribu kuwahamasisha wachezaji kujitambua wenyewe kwamba wanaichezea klabu kubwa Manchester United. Lakini kiukweli hicho si kitu kinachoweza kusaidia ushindi kwa mechi nyingi au uwezekano wa kutwaa mataji.

Mara zote United imekuwa ni kama kiongozi wa klabu nyingine kwenye suala la uongozi na ndio maana ikapitiwa na makocha bora duniani kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita. Lakini staili ya uongozi wa kocha wa sasa ya kupaniki pale matokeo yanapokuwa tofauti na matarajio yake, kunaifanya klabu hiyo kuzidi kuanguka.

Ni wazi kwamba, Solskjaer huwezi kumlinganisha na Pep Guardiola au Jurgen Klopp hata Maurizio Sarri, kwa sababu watu hao wameshinda mechi nyingi si tu kwa sababu ya uongozi bora, lakini ni kwa sababu ya mbinu na mipango yao.

Ni wakati sasa kwa United kuteua kocha ambaye anajua kushinda kila kitu kwenye kila mchezo uwanjani.

**1. UDHAIFU SAFU YA USHAMBULIAJI**

Ni wazi kwamba maisha ya Alexis Sanchez hapo United yamekuwa yasiyo na mafanikio na Romelu Lukaku ameshindwa kuthibitisha ubora wake wa kuisaidia United. Pengine ndio maana alishindwa kuwika pale Chelsea.

Kiwango cha Rashford kimekuwa cha kusuasua msimu huu hapo United, na hakuna shaka kwamba, majaliwa ya baadaye ya mshambuliaji huyo kijana wa Uingereza yanaweza kuwa gizani. Mwazo alionekana kama ni mchezaji mwenye muonekano wa kuwa na majaliwa mazuri siku za usoni hapo United. Lakini kwa sasa hajawa mshambuliaji mwenye msaada mkubwa kama ilivyo kwa Salah au Diego Costa au hata Aguero.


Kiwango cha Lukaku na Rashford hakitoshi kuichezea klabu kubwa kama United ambayo inahitaji wachezaji wenye majina makubwa kuweza kuirudisha kwenye nafasi yake ya awali.

Safu ya kiungo kuna wakati inaonekana kama imeimarika ikiongozwa na mchezaji ghali wa klabu hiyo, Paul Pogba.

Pogba anaweza kufunga mabao machache kama ilivyo kwa Herrera, lakini Fred, Matic au McTominay wameshindwa kabisa kuonyesha uwezo wao wa kuisaidia timu katika kufunga mabao ambayo yataipaisha klabu hiyo hadi sasa.

Kwa uhakika kabisa United inahitaji mshambuliaji ambaye anaweza kufunga mabao 10 hadi 15 ambayo yataisaidia klabu hiyo kuwa na wastani mzuri wa kufunga mabao zaidi katika kila mchezo.

**NDANI YA 18**



BAO la 1,000 kwenye Ligi Kuu England msimu huu limefungwa na beki wa kushoto wa Southampton, Matt Targett, juzi, wakati wakitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Bournemouth, aidha, katika ligi hiyo bao la 1,000 la mapema zaidi lilifungwa msimu wa 1994-95 (Aprili Mosi,1995).

MSIMU wa sasa wa Ligi Kuu ya England umekuwa mmoja kati ya unaoburudisha zaidi katika siku za hivi karibu. Manchester City na Liverpool zinapigana vikumbo kuwania taji hilo, huku Tottenham Hotspur, Arsenal, Chelsea, na Manchester United zikijaribu kuipigania nafasi nne za juu.
**Uk. 16-17**



# MBAPPE ANAPOWAPIKU RONALDO, MESSI

**PARIS,** Ufaransa

MABAO matatu 'hat-trick' ya Kylian Mbappe kwa Paris Saint-Germain wakati ikiifunga Monaco Jumapili, yalimfanya kucheka na nyavu mara 30 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Umekuwa ni msimu mzuri zaidi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye alikuwa na wakati mzuri kwenye Kombe la Dunia na hakuna mchezaji mwenye umri chini ya miaka 21 aliyeweza kufunga idadi hiyo ya mabao kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu za Ulaya, tangu gwiji wa Brazil, Ronaldo alipofanya hivyo wakati akiwa na umri wa miaka 24.

Lakini kwa vipi Mbappe ameweza kufaya hivyo tofauti na wakali wengine kama Lionel Messi, Cristiano Ronaldo na Zlatan Ibrahimovic wakati wakiwa na umri huo?

Hapa tunawaangalia wachezaji waliofunga idadi kubwa ya mabao kwa msimu kabla hawajafikisha umri wa miaka 21, twende sasa...

**EPL: NYOTA WA LIVERPOOL WALIANZISHA**

Ligi Kuu ya England imekuwa moja ya ligi bora barani Ulaya inayozalisha vipaji vya ukweli kwa miaka kadhaa, pamoja na kuwa kivutio cha wachezaji wenye vipaji vya ukweli duniani.

Cristiano Ronaldo alifunga mabao 14 kwenye ligi hiyo kabla hajafikisha umri wa miaka 21, huku mchezaji mwenzake wa Manchester United, Wayne Rooney akifunga mabao 44. Wachezaji wengine ambao walikuwa vijana na walifunga mabao mengi ni pamoja na Romelu Lukaku, Nicolas Anelka na Chris Sutton.

Lakini walikuwa nyota wa zamani wa Liverpool ambao walifunga mabao mengi kabla ya kufikisha umri wa miaka 21. Michael Owen alifunga mabao 55 kabla ya Desemba 14, mwaka 2000, huku Robbie Fowler akifunga mabao 64 kutoka mwaka 1993 hadi 1996.

Kipindi kizuri zaidi kwa Fowler kilikuja msimu wa mwaka 1995-96, wakati alipotikisa nyavu mara 28 wakati Liverpool ilipomaliza nafasi ya tatu, ingawa mabao yake ya mwisho yalikuja baada ya kufikisha umri wa miaka 21.

**LIGUE 1: MBAPPE NDIYE KILA KITU**

Kylian Mbappe anakwenda kasi zaidi na tayari ana mabao 58 kwa jina lake.

PSG imekuwa ikimtegemea kijana huyo kwenye ufungaji wa mabao kwa kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel msimu huu na kuongoza kwenye mbio za ubingwa wa Ligue 1, huku akiwa bado hajafikisha umri wa miaka 21.

Gwiji wa Ufaransa, Michel Platini alifunga mabao 22 kwa klabu yake ya Nancy msimu wa 1975-76, huku Djibril Cisse akifunga idadi kama hiyo ya mabao msimu wa 2001-02 akiwa na Auxerre.

Karim Benzema, pia alifurahia wakati wake akiwa amefunga mabao 20 msimu wa 2007-08 akiwa pale Lyon.

**LA LIGA: RAUL ANAONGOZA**

Si mara kwa mara Lionel Messi akijikuta mwenyewe kama ndiye bora, lakini kwenye suala la rekodi yake ya kufunga mabao 31 kabla ya kufikisha umri wa 21, inamfanya kuwa kwenye orodha ya wafungaji vijana wenye historia ya aina yake pale La Liga.

Messi hakuwa akicheza kama mshambuliaji wakati alipoanza kuonyesha cheche zake pale Camp Nou katika msimu wa 2006-07, wakati alipofunga mabao 14.

Nyota wa Atletico Madrid, Fernando Torres na Sergio Aguero wote walifunga mabao 19 wakati wakiwa kwenye ubora wao kabla ya kufikisha umri huo.

Lakini Atletico ilishuhudia mchezaji kijana kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Real Madrid. Raul alifunga mabao 59 kabla hajafikisha umri wa miaka 21, yakiwamo mabao 21 katika mechi 42 alizocheza msimu wa 1996-97.

**BUNDESLIGA & SERIE A: WERNER NA ICARDI**

Klaus Fischer, Horst Koppel na Dieter Muller wote walikuwa na wakati mzuri kipindi chao cha ujana kwenye Ligi Kuu ya Ujerumaani, Bundesliga, ingawa mabao yao waliyafunga miaka ya 1960 na 1970.

Tangu wakati huo, vijana hao wamekuwa na wakati mgumu kufunga mabao mengi Ujerumani, huku nyota wa RB Leipzig, Timo Werner akifunga mabao 14 wakati akikaribia kufikisa umri wa miaka 21 msimu wa 2016-17.

Kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Mauro Icardi alifunga mabao 10 kwa Sampdoria msimu wa 2012-13 kabla ya kuondoka Inter, ambako alifunga mara tisa.

**EREDIVISIE: RONALDO NA MAGWIJI WA AJAX**

Mchezaji wa mwisho chini ya umri wa miaka 21 kufunga mabao 30 kwa msimu mmoja kabla ya Mbappe alikuwa ni Ronaldo msimu wa 1994-95, huku akifunga mabao hayo akiwa na umri wa miaka 18.

Wakati Ronaldo alionyesha uwezo huo akiwa pale PSV, alikuwa nyota wa Ajax, Johan Cruyff alifunga mabao 33 msimu wake wa 1966-67.

Na Ajax pia walizalisha wachezaji watatu zaidi; Wim Kieft (33), Marco van Basten (27) na Patrick Kluivert, ambaye alifunga mabao 18 katika msimu wake wa 1994-95, na kuwasaidia miamba hao wa Amsterdam kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya.

Zlatan Ibrahimovic alihama kutoka Malmo kwenda Ajax akiwa na umri wa miaka 19 na alifanikiwa kufunga mabao sita katika msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi.

**USILOLIJUA**

TANGU kuanza msimu wa 2016-17, kiungo wa Watford, Mgiriki Jose Holebas, ameonyeshwa kadi za njano 33 kwenye Ligi Kuu England, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote katika ligi hiyo.



## Wamuomba JPM kuingilia kati bwawa la Lwanyo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

IKIWA zimebaki siku chache Rais Dk. John Magufuli kufanya ziara katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Igurusi wilayani humo wamemuomba aingilie kati ujenzi wa bwawa la umwagiliaji la Lwanyo, ambalo linajengwa kwa zaidi ya miaka mitano bila kukamilika huku wakulima wa mpunga waliokuwa wamelengwa wakiendelea kupata shida.

Walitoa kilio hicho juzi wakati wa mkutano maalumu wa chama ngazi ya kata uliolenga kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM kutoka kwa Diwani wa Kata ya Igurusi, Hawa Kiwele, ambaye ni diwani wa kwanza mwanamke wa kata hiyo.

Katibu Mwenezi wa CCM wa Kata ya Igulusi, Pili Ibrahim, alisema diwani wa kata hiyo amejitahidi kutekeleza ilani, lakini bado kuna changamoto kubwa ya kitaifa ya bwawa la umwagiliaji la Lwanyo, ambalo likikamilika litaongeza uzalishaji wa zao la mpunga na vitunguu katika kata hiyo pamoja na maeneo jirani.

Alisema bwawa hilo likikamilika litasaidia kata za Igurusi na Utengule Usangu, kwenye kilimo cha umwagiliaji pamoja na kupunguza migogoro ya matumizi ya maji ya Mto Ruaha, ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara wilayani humo. "Kilio chetu kikubwa katika Kata hii ni bwawa hili kwa kuwa ni muda mrefu umepita halina manufaa yoyote kwa wananchi na ujenzi wake unasuasua na hata uimara wake sio wa uhakika, hivyo tunamuomba rais wetu aingilie kati ili likamilike haraka," alisema Pili. Diwani wa Kata ya Igurusi, Kiwele alisema katika kata yake ametekeleza ilani kwa asilimia 90, lakini kumekuwapo na tatizo ambalo wananchi wanalalamika kila siku kuhusu bwawa hilo kushindwa kukamilika kwa muda muafaka.

Kiwele alisema bwawa la umwagiliaji la Lwanyo lina zaidi ya miaka mitano tangu ujenzi uanze bila kukamilika, wakati linadaiwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni tatu zimeteketea na kwamba lilikuwa likisimamiwa na Wizara ya Maji kupitia Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji Mbeya. "Hii imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi kutokana na kuwa na matumaini ya kuweza kuendelea kulima na kuinuka kiuchumi, lakini hadi sasa ndoto za wakulima zinazidi kupungua kwa kuwa walitegemea kunufaika na bwawa hilo," alisema Kiwele. Naye, Amos Mwakalinga, alisema baada ya serikali kuweka mkakati huo wa kutengeneza bwawa hilo, ndoto ya vijana wengi ilikuwa ni kujiinua kiuchumi kupitia mradi huo, lakini kwa sasa imegeuka giza.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti (kushoto), akipongezwa na mkazi wa Kijiji cha Irkujit Kata ya Edonyongijape wilayani Simanjiro, Thomas Laizer, baada ya kuendesha harambee ya papo kwa papo na kupatikana Sh. milioni 17 za ujenzi wa zahanati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# JPM abaini miradi hewa ya maji zaidi ya bil. 200/-

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MIRADI ya maji iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 100 nchini, imebainika kuwa ilikuwa hewa na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo zimeliwa na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Maji.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Chunya, mkoani Mbeya na Rais Dk. John Magufuli, alipokuwa anawahutubia wananchi wa Wilaya ya Chunya kwenye viwanja vya Sabasaba baada ya kutolewa taarifa ya kukamilika kwa mradi wa maji uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 900 siku moja kabla ya kufanya ziara wilayani humo.

Alisema ana wasiwasi na taarifa za mradi huo kukamilika na hivyo atatuma wataalamu wake kwa ajili ya kwenda kuchunguza mradi huo ili kujua ukweli huku akimtaka Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, kuhakikisha anafuatilia miradi yote ya maji ili kuhakikisha inawanufaisha wananchi.

"Kwanini mradi ukamilike wakati nakuja mimi huku, ulikuwa wapi kukamilika siku zote? Sasa nina wasiwasi, nitachunguza na nitaujuwa ukweli, watendaji wa Wizara ya Maji wamekuwa wakidanganya miradi mingi, kati ya miradi ya Sh. bilioni 116 ni 16 pekee ndiyo ilikuwa halali, mingine yote ilikuwa hewa," alisema Rais Magufuli.

Aidha, alisema Chunya ni miongoni mwa wilaya kongwe nchini, lakini inakabiliwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu kutokana na miradi yake kutokamilika haraka hivyo kuwataka wataalamu kuhakikisha wanakamilisha miradi yote haraka ili kuwaondolea adha wananchi wa wilaya hiyo.

Akitoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa maji wilayani Chunya, Waziri wa Maji, Prof. Mbarawa alisema mahitaji ya maji kwa siku katika wilaya hiyo ni lita milioni nne, lakini uzalishaji uliopo ni lita 362,000 hivyo wanategemea miradi inayoendelea kutekelezwa ikikamilika itasaidia kumaliza changamoto iliyopo.

Alisema mradi uliogharimu Sh. milioni 900 tayari umekamilika na maji yameanza kutoka, lakini changamoto iliyopo ni uchakavu wa miundombinu ambayo ni ya muda mrefu na hivyo wanakusudia kununua mabomba mapya.

"Wilaya hii ni miongoni mwa 24 nchini zitakazonufaika na mkopo wa India na tunatarajia kutekeleza mradi utakaokuwa unazalisha lita milioni nane na ndio utakuwa suluhisho la changamoto ya maji katika wilaya hii," alisema Prof. Mbarawa.

Aidha, alisema ujenzi wa Bwawa la Matwiga ambalo litawanufaisha wananchi zaidi ya 50,000 kutoka katika vijiji 16 umekamilika kwa asilimia 91 na muda sio mrefu maji hayo yataanza kusambazwa kwa wananchi wa maeneo hayo.

Vilevile alisema serikali imetoa fedha zingine zaidi ya bilioni mbili kwa ajili ya miradi mingine ya maji katika wilaya hiyo ya Chunya.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Lupa, Victor Mwambalaswa, alisema tatizo la maji wilayani humo ndiyo inayokisumbua hata Chama cha Mapinduzi wanapoenda kwa wananchi kuelezea mambo yanayofanywa na serikali yao.

Aliiomba serikali kukamilisha haraka mradi wa maji wa Bwawa la Matwiga ili wananchi wa vijiji 16 vinavyolengwa viondokane na changamoto ya maji inayowakabili kwa sasa.

# Tulia Trust kujenga mabweni ya wasichana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust inayomilikiwa na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, inakusudia kutumia fedha zitakazokusanywa kupitia mashindano ya mbio yanayotarajiwa kufanyika Mei 4, mwaka huu jijini Mbeya, kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike kwenye shule za kata jijini Mbeya.

Hayo yalisemwa juzi na Dk. Tulia alipokuwa anazungumza na wandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mashindano hayo na kusema tangu mashindano hayo yalipoanza mwaka 2017, fedha zinazokusanywa zimekuwa zikitumika kuboresha miundombinu ya elimu na afya katika mkoa huo.

Mwaka wa kwanza wa mashindano hayo fedha zilizokusanywa zilitumika kuboresha mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Loleza ya jijini Mbeya pamoja na kujenga vyoo na mabafu kwenye wodi ya wazazi ya Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana.

Alisema kwa mwaka huu anakusudia kuwasaidia watoto wa kike wanaosoma kwenye shule za sekondari ambao wanakabiliwa na changamoto za kutembea umbali mrefu kwenda shuleni hali inayosababisha kukumbana na vishawishi vinavyowafanya wapate mimba na kukatisha ndoto zao.


"Mpaka sasa tumepokea maombi kutoka shule nyingi, lakini tutakachokipata tutasaidia shule zenye uhitaji zaidi, sio kwamba zingine hatutazisaidia, lakini tutakuwa tunaendelea mwaka hadi mwaka kwa sababu haya mashindano ni endelevu," alisema Dk. Tulia.

Alisema maandalizi ya mashindano hayo yameshakamilika na wakimbiaji mbalimbali wameshajiandikisha kushiriki mashindano hayo wakiwamo wa ndani na nje ya nchi na washindi watapata zawadi mbalimbali.

Alisema mpaka sasa wamejiandikisha washiriki zaidi ya 1,200 wakiwamo baadhi ya mawaziri ambao watashiriki mbio fupi ambazo hazina zawadi na zitakuwa kwa ajili ya kujifurahisha na kuimarisha afya zao.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha mbio ndefu za Kilomita 42 na kilomita 21 kwa wanaume na wanawake na za mbio fupi za kilomita mbili ambazo zitawahusisha watu wa makundi maalumu wakiwamo wenye ulemavu, wazee na watoto wa shule za msingi.

Dk. Tulia alisema mashindano hayo yataanza kwa washiriki kwenda kushiriki chakula cha pamoja kitakachoandaliwa Mei 3 katika eneo la Mlima Kawetere, Barabara ya Mbeya - Chunya ili kuwaandaa washiriki hao.





# Sekta binafsi yachangia ajira kibao

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema sekta binafsi nchini imechangia kuziba pengo la ajira kwa kuzalisha ajira 137,054 sawa na asilimia 28, huku sekta ya umma ikiongoza kwa ajira 345,547 sawa na asilimia 72.

Hata hivyo, kiwango cha juu cha uzalishaji wa ajira katika sekta ya umma kimetokana na utekelezwaji wa miradi ya maendeleo.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, alipokuwa akizungumza na watu wenye ulemavu na wadau mbalimbali wakati wa tamasha la uimbaji lililoandaliwa na Tanzania Music Foundation.

Alisema Serikali inaendelea na jitihada zake za kuhamasisha wadau mbalimbali kuandaa na kutekeleza programu za kukuza ajira nchini.

Kwa mujibu wa Ikupa, sekta hizo zilichangia kupunguza pengo hilo la ajira katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Alisema kutokana na jitihada hizo za serikali kwa watu wenye ulemavu wameweza kupatiwa ajira na wengine kuwezeshwa kwenye ujasiliamali na kufanikiwa kujitegemea kama ilivyo kwa wengine wasiokuwa na ulemavu.

Aidha, alisema ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaondokana na baadhi ya changamoto serikali pia haitawaacha nyuma kimaendeleo bali itaendelea kuwawezesha kuishi maisha ya kujitegemea kwa kuwa tayari imeshatunga sheria ya fedha ya mwaka 2018.

Alisema kuwa sheria hiyo ikiwa ni ya kuzitaka halmashauri zote nchini kutenga asilimia mbili ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu katika shughuli za kiuchumi ili mikopo hiyo utolewe bila riba yoyote.

Naibu waziri huyo alisema kupitia matamasha mbalimbali ya uimbaji yamekuwa yakiisaidia serikali katika uelimishaji kwa jamii juu ya kupinga vitendo vya unyanyasaji na ukatili wanaofanyiwa watu wenye ulemavu.

Naye, Rais wa Tanzania Music Foundation, Dk. Donald Kisanga, aliiomba serikali kuhakikisha inatoa ajira kwa watu wenye ulemavu kwa wale wenye sifa ya elimu na ujuzi ili kuwapunguzi makali ya changamoto walizokuwanazo.

# Wafanyabiashara waiangukia serikali mifuko ya plastiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UMOJA wa wafanyabiashara wa vifungashio mkoa wa Dodoma, wameiomba serikali kuwaongezea muda wa miezi nane kuendelea kuitumia mifuko ya plastiki kutokana na wengi wao kuwa na mzigo mkubwa katika maghala yao.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa umoja huo, Robson Rober, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema wao kama wafanyabiashara wa Mkoa wa Dodoma kwanza wanaipongeza Serikali kwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ili kulinda mazingira na afya za watu pamoja na mifugo.

"Tunaomba sana serikali ituongezee muda kidogo angalau miezi nane ambayo tunaona inatosha kulingana na mzigo tulionao katika stoo zetu," alisema Robert.

Robert aliongeza kuwa, wanaomba kuongezewa muda huo kutokana na wengi wao kuwa na mzigo mkubwa kwenye maghala yao ambao hauwezi kuisha kwa muda waliopewa.

"Lakini pia wafanyabiashara wengi tunaendesha biashara kwa mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za kifedha, hivyo huu mzigo tulionao katika stoo zetu ukiteketezwa mara baada ya muda tuliopewa kuisha, tutabaki na madeni ambayo hatuwezi kuyalipa," alisema.

Aidha, alisema wanaomba muda kuongezwa kutokana na vifungashio mbadala wanavyotarajia kuviuza kwa muda huo uliopangwa na serikali havitaweza kukidhi mahitaji ya nchi kwa haraka badala yake magazeti ambayo kiafya ni sumu yanaweza kutumika pamoja na mifuko ya karatasi ambayo ni rahisi kutengenezwa kienyeji.

Pia alisema mifuko hiyo imeajiri vijana wengi ambao wataathirika mitaji yao kama muda hautaongezwa maana bado watakuwa hawajabadilisha mitaji yao toka kwenye mifuko ya plastiki kwenda kwenye vifungashio mbadala.

"Tunaomba viwanda kwanza viache kuzalisha mifuko hiyo ya plastiki hiyo Mei 31, mwaka huu ili mifuko ya plastiki ambayo ipo kwenye mzunguko imalizike na wakati huo viwanda viwe vinazalisha mifuko mbadala," alisema.

Hivi karibu serikali kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ilitangaza kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini ifikapo Juni 1, 2019.

Baada ya kutangaza katazo hilo la mifuko ya plastiki, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, akizungumza na vyombo vya habari alisema uamuzi huo umekuja wakati sahihi.

Makamba alisema maamuzi hayo yaliyofanywa wa serikali yalijumuisha wadau ili kuona namna bora ya matumizi ya mifuko mbadala na kuachana na mifuko ya plastiki.

"Kama hatuta acha kupiga marufuku ya mifuko hii ya plastiki watafiti wanasema kuwa ifikapo 2050 idadi ya mifuko itakuwa mingi baharini kuliko idadi ya samaki waliopo lakini inaharibu sana mazingira," alifafanua

Makamba. Hatahivyo, alisema serikali tayari ilishafanya utafiti wa kina na kujiridhisha kuwa uzalishaji wa mifuko mbadala utaweza kutosheleza mahitaji ya nchi baada ya Juni 1, mwaka huu wakati ambapo katazo hilo litaanza kutekelezwa.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu (kulia), Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Martin Busungu, wakisaini Mkataba wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: WMN**

# Mbunge ataka kasi utoaji vitambulisho vya Taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, ameiomba serikali kuongeza kasi ya utoaji wa vitambulisho vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kupata kitambulisho hicho.

Akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2019/20 mwishoni mwa wiki,

Kigua alisema utoaji wa vitambulisho hivyo unafanyika kwa kasi ndogo.

"Zoezi hili linakwenda taratibu, juzi tumepata taarifa kwamba Mei mosi, mwaka huu kila mwenye kitambulisho cha Taifa ndiyo atakayesajiliwa laini, sasa hili ni tatizo,"alisema.

Alifafanua kuwa Wizara hiyo iliingia mkataba na kampuni ya Iris Corporation iliyosainiwa Septemba mwaka 2014 na mkataba ulikuwa hadi 2016 wa kutengeneza vitambulisho lakini uliongezwa hadi Septemba mwaka jana jambo ambalo linapaswa kufanyiwa kazi na wizara husika.


"Vitambulisho vya Taifa ni haki ya kimsingi ni lakini muongeze 'Speed' ili kuhakikihsa kwamba vinapatikana kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa na nalisema hili maana tunapata malalamiko huko vijijini kwamba bado,"alisema Kigua. Aidha aliipongeza Wizara hiyo kuwa kupitia jeshi la polisi wameweza kupunguza ajali na uhalifu.

Alisema zamani watu walikuwa wanashuhudia uhalifu unafanyika katikati ya Dar es Salaam lakini kwasasa vitendo hivyo vimepungua. Pamoja na hayo,

Kigua alipongeza wizara hiyo kwa jitihada inazochukua kuhakikisha vinajengwa vituo vya polisi pamoja na magereza. "Changamoto ni kubwa kila maeneo hususani kwa wilaya mpya, na mimi nikushukuru mheshimiwa Waziri kwakuwa tumepata Sh.Milioni 150 kwa ajili ya kujenga nyumba za polisi Wilaya ya Kilindi,"alisema.

Alisema bado wilaya yake ya Kilindi kuna changamoto ya kituo cha kisasa kwakuwa wilaya hiyo ni ya muda mrefu tangu mwaka 2002.

Alimwomba Waziri aiangalie wilaya hiyo ili iwe na kituo cha kisasa cha polisi na kwamba vituo vya kata vilivyobaki watajenga wenyewe.





Trafiki wakiwa kazini maeneo ya Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, ili kuhakikisha madereva wanazingatia Sheria za Usalama Barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Dk. Shein mgeni rasmi Mei Mosi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, Jumatano anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani yanayotarajiwa kufanyika Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Wanawake na Watoto, Modlin Castiko, alisema chimbuko la maadhimisho hayo ni kukumbuka mgogoro uliotokea Chicago, Marekani kati ya ya waajiri na wafanyakazi.

Alisema chimbuko hilo lilifuatia baada ya wafanyakazi kudai kupunguziwa muda wa kufanyakazi kutoka saa 15 ya kazi kwa siku hadi saa nane kwa siku.

Alisema madai hayo yalisababisha mgomo mambao uliwakasirisha sana waajiri na kuchukua hatua kali dhidi ya wafanyakazi hao. Alieleza miongoni mwa hatua hizo zilizochukuliwa ni pamoja na waajiri walitumia askari ili kuvunja mgomo huo ambapo askari hao walitumia nguvu na kupelekea kuumia kwa wafanyakazi na wengine kupoteza maisha.

Waziri Castico alisema tangu wakati huo dunia imejifunza kuwa ili kuleta maendeleo katika sekta ya kazi, mashauriano na majadiliano ndio jambo la msingi na si kutumia nguvu, wadhifa au taasisi.

Aidha, aliwataka wafanyakazi kufanya kazi kwa ufanisi, uweledi na uadilifu ili kuleta tija itakayokuza na kuleta faida kwao wao wenyewe, waajiri na taifa kwa ujumla.

Naye Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), Khamis Mwinyi, alisema watahakikisha wanawasaidia wafanyakazi wanaokumbwa na matatizo katika sehemu zao za kazi ili kutetea maslahi yao.

Alisema baadhi ya wafanyakazi wanapata matatizo mengi kweye maeneo ya kazi, lakini wanahofia kufukuzwa kazi pindi wakitoa taarifa juu ya matatizo yanayowakabili, jambo ambalo hupelekea kukosa haki zao kisheria na kupoteza maslahi yao. Mwenyekiti wa ZATUC, Hassan Silima, alisema utafiti mbalimbali umefanyika katika taasisi zinazoajiri wafanyakazi na kubaini bado kuna tatizo la kucheleweshewa mishahara wafanyakazi, posho, mazingira magumu katika kazi na mambo mengine ya udhalilishaji.

Aliwataka wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kueleza changamoto zinazowakabili na kupatiwa ufumbuzi.

Ujumbe wa mwaka huu katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi ni kuimarika kwa uchumi wa taifa kuendane na kuongezeka kwa maslahi ya wafanyakazi.

# Waziri asisitiza wanafunzi masomo sayansi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wa masomo ya sayansi, kuyatumia kwa vitendo mafunzo waliyopata ili taifa liweze kuzalisha wataalamu bora.

Akifunga kambi ya mafunzo ya Sayansi ya vitendo kwa wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Unguja na Pemba katika viwanja vya Chuo cha Sayansi za Afya Mbweni, alisema masomo ya sayansi ni kujifunza uhalisia wake na kujua mazingira ya maisha ya kila siku.

Alisema upo umuhimu wa kufanya bidii ya hali ya juu ya kufundisha masomo ya sayansi kwa vitendo ili taifa lipate wataalamu wa fani mbalimbali za sayansi.

Riziki aliwataka wanafunzi hao kuyatumia mafunzo waliyoyapata ili kujiongezea uelewa pamoja na kuwaelemisha wanafunzi wenzao ili kufaidika na wao kupata wataalamu zaidi.

Aidha, aliwataka walimu wanapofundisha masomo ya sayansi kutumia lugha nyepesi pamoja na kutumia vifaa kwa uhalisia ili kuwawezesha wanafunzi kufahamu kwa haraka zaidi.

Naye Meneja miradi kutoka Umoja wa Wanawake Wasomi wa Afrika ( FAWE), Hinda Abdullah Ajmy, alisema lengo la kuweka kambi hiyo ni kuhamasisha wanafunzi hasa wa kike kusoma na kuyapenda masomo ya sayansi kutokana na wanafunzi wa kike kutoyapenda masomo hayo.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia wanafunzi kujijua na kuitumia sayansi kwa lengo la kukuza vipaji na ujuzi wao na kusaidia taifa kuwa na wanasayansi wengi hasa wanawake.

Mwakilishi wa Shirika la Milele Zanzibar Foundation, Ali Mohamed Abdallah, alisema kupitia shirika hilo watahakikisha wanakuza sekta ya elimu kwa kuwahamasisha wadau mbalimbali kuekeza kwenye elimu hasa masomo ya sayansi.

Mafunzo hayo ya siku saba yanayojulikana kama "STEM for Success" yameandaliwa na FAWE kwa kushirikiana na Milele Foundation na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), yameshirikisha shule 15 za sekondari, tisa kutoka Unguja na sita kutoka Pemba ambapo jumla ya wanafunzi 150 walishiriki.

## Kada ajitapa CCM kushinda mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Leila Burhan Ngozi, amedai hakuna chama kitakachozuia ushindi wa CCM ngazi zote katika Jimbo la Malindi katika uchaguzi mkuu ujao.

Akizungumza baada ya matembezi ya kuimarisha uhai wa chama hicho, alisema mwaka 2020 ndio wakati mwafaka wa kulikomboa Jimbo hilo lirudi CCM, hatua itakayopelekea wananchi wa eneo hilo kuendelea kunufaika na matunda ya Serikali ya CCM.

Alisema CCM ina nafasi ya mwakilishi na madiwani katika jimbo hilo na kwa nafasi ya ubunge imeshikiliwa na upinzani, hali inayopelekea kutokuwapo kwa ushirikiano katika utekelezaji wa ilani ya CCM.

Alisema ridhaa ya kulitwaa Jimbo hilo kuwa la CCM itatoka kwa wananchi wenyewe ambao wameonyesha nia ya kuiamini CCM.

Alieleza CCM inajivunia utekelezaji mzuri wa ilani yake katika maeneo mbalimbali nchini likiwamo Jimbo la Malindi.

Alisema kasi ya CCM ya kuwapelekea wananchi maendeleo endelevu itaendelea kuongezeka kila siku kabla na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, kwa kuwa wananchi wanataka maendeleo na sio maneno ya porojo na ahadi hewa.

Alizitaka jumuiya zote za CCM kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa mujibu wa kanuni na miongozo yao ili mwaka 2020 CCM ishinde kwa kishindo.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa za kielimu zilizopo nchini sambamba na kujiunga na vituo mbalimbali vya ufundi ili wapate ujuzi na utaalamu wa kuwawezesha kujiajiri.

"Serikali zetu zipo katika safari ya kutafsiri kwa vitendo sera ya uchumi wa viwanda kwa kuamrisha viwanda vidogo na vikubwa vifanye kazi ili wananchi wapate ajira, lakini pia tuzalishe bidhaa nyingi na kuuza nje ya nchi kwa lengo la kuingiza fedha za kigeni," alisema Leila.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Mjini, Hudhaima Mbarouk Tahir, aliwashukuru vijana walioshiriki katika matembezi hayo.

Hudhaima alieleza kuwa matembezi hayo yatakuwa endelevu katika majimbo mbalimbali yaliyopo katika wilaya hiyo kwani ni sehemu ya kuwaunganisha vijana na kuwajenga kuwa wazalendo.

HABARI KIMATAIFA

## Ebola yaua watu 900 kwa miezi tisa

**KINSHASA,** Congo

UGONJWA Wa Ebola umesababisha vifo vya watu 900 tangu mwezi Agosti mwaka jana katika eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambako ukosefu wa usalama na uasi vimesababisha ugumu katika mapambano kwa mujibu wa mamlaka za afya nchini humo.

Tangu mwanzo wa mlipuko wa ugonjwa huo, matukio 1,396 viliripotiwa ikiwamo 1,330 vilivyothibitika na kati ya hivyo 66.

Wakati DRC ikipambana na mlipuko wa pili mkubwa wa ugonjwa wa Ebola, Shirika la Umoja wa Mataifa la mpango wa chakula duniani (WFP) lilitahadharisha hivi karibuni kuwa rasilimali zinazohitajika kusaidia shughuli zake haziendani na kasi ya ongezeko la maambukizi na uwepo wa hatari ya kusambaa kwa virusi hivyo ndani ya DRC na katika nchi za jirani. **RFI**

## Polisi wawatawanya walimu

**RABAT,** Morroco

ZAIDI ya waandamanaji 70 wamejeruhiwa baada ya polisi katika Mji Mkuu wa Morocco Rabat, kutumia maji kutawanya mkusanyiko wa maelfu ya walimu waliokuwa wakiandamana wakilalamika dhidi ya kanuni za mikataba yao ya kuajiriwa.

Walimu hao walikuwa wakipaza sauti zenye ujumbe wa kutaka haki ya kijamii na kupinga uongozi mbovu katika shule za uma.

Walimu hao walipiga kambi nje ya bunge lililopo katikati mwa Jiji la Rabat, wakitaka matakwa yao kushughulikiwa, lakini polisi walitumia nguvu kuvunja maandamano hayo.

Walimu katika shule za umma wengi wao wakiwa wamevalia makoti meupe walitoka miji tofauti nchini humo kwa maandamano hayo, baada ya mkutano uliokuwa umepangwa baina yao na maafisa wa wizara ya elimu kuahirishwa siku ya Jumanne.

Zaidi ya walimu 55,000 walioajiriwa kwa kandarasi za muda mwaka 2016, walianzisha mgomo machi mwaka huu na kufanya maandamano makubwa ili kuhimiza matakwa yao yatekelezwe ya kuajiriwa kwa mikataba ya kudumu ili kuboresha hali yao hasa watakapostaafu.

Walimu wanaofanya kazi kwa mkataba wa mda mfupi nchini Morocco wanalipwa dola za Marekani 520, sawa na wenzao walioajiriwa kwa mkataba wa kudumu, lakini hawapokei marupurupu yoyote, ikiwamo malipo ya pensheni. **VOA**

# Xi apigia chapuo mradi wa miundombinu

**BEIJING,** China

RAIS wa China, Xi Jinping, amezitaka nchi zaidi duniani zijiunge na mradi wa nchi yake wa ujenzi wa miundombinu, mpango ambao Marekani inahofia unajenga ushawishi mkubwa zaidi wa kimkakati kwa manufaa ya China.

Rais Xi ametoa wito huo katika mkutano wa pili wa kilele kuhusu mradi wa China wa ujenzi wa miundombinu ya kuyaunganisha mabara unaofanyika mjini Beijing, ambao viongozi wengine wameelezea hatua yao ya kuunga mkono mradi huo.

Mkutano huo wa kilele ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa serikali na kuhudhuriwa na viongozi wa nchi zaidi ya 40, wakiwamo wa kutoka nchi za Afrika.

**Mkutano huo wa kilele ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa serikali na kuhudhuriwa na viongozi wa nchi zaidi ya 40, wakiwamo wa kutoka nchi za Afrika.**

Rais wa Urusi, Vladmir Putin na viongozi wengine wa ulimwengu wameupongeza mradi huo, hatua inayoonekana kama pigo kwa utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump ambao unajaribu kuzikatisha tamaa nchi nyingine zishiriki katika mpango huo.

Juzi wakati akiufungua mkutano huo, Rais Xi alijaribu kuondoa wasiwasi kwa washiriki na kuwaeleza kuwa siyo kweli kwamba mradi huo utaziingiza nchi mbalimbali katika mtego wa madeni.

Aidha, alikanusha madai kwamba mradi huo hauziendelezi nchi za Afrika na za barani Asia ambazo zimejenga bandari na njia za reli kwa mikopo kutoka China. Katika hotuba yake, Rais Xi aliahidi kuwa nchi yake inadhamiria kuleta faida kwa wote.

"Tunahitaji kuhimiza kuhusu ushiriki kamili wa nchi zaidi pamoja na makampuni," alisema Rais Jinping.

Hayo yanajiri wakati ambapo Rais Jinping alisema mikataba yenye thamani ya Dola bilioni 64 imesainiwa siku ya jumamosi ambayo ni siku ya pili katika mkutano huo.

Akizungumza wakati akiufunga mkutano huo, Rais Jinping alirudia na kueleza kuwa mradi huo mkubwa wa Trilioni za Dola unaohusisha ujenzi wa barabara, madaraja, mabomba na bandari, utazingatia uwazi na maendeleo ya mazingira safi na pande zote zitashiriki katika msingi wa haki sawa.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na viongozi wanaohudhuria mkutano huo imeelezea kufurahishwa na fursa muhimu zilizoanzishwa kupitia mradi wa ujenzi wa miundombinu na wamesema unasaidia katika kupatikana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Washiriki hao ni pamoja na marais kutoka Ufilipino, Kenya na Misri, Waziri Mkuu wa Italia, Ugiriki na Pakistan pamoja na maafisa wengine wa serikali kutoka Indonesia, Ujerumani na nchi nyingine. **DW**



Mishumaa ikiwa imewashwa katika moja ya Kanisa la Presbyterian, kuomboleza kifo na majeruhi wa shambulio la risasi lililotokea katika Sinagogi Kaskazini mwa mji wa San Diego. **PICHA: REUTERS**

# Auawa kwa risasi ndani ya sinagogi

**CALIFORNIA,** Marekani

MTU mmoja ameuawa na wengine watatu kujeruhiwa baada ya mtu mwenye silaha kuingia katika sinagogi mjini Poway, Jimbo la California na kuanza kuwashambulia.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Mkuu wa polisi wa Kaunti ya San Diego, Bill Gore alisema mwanaume mmoja aliingia katika sinagogi majira ya saa 5:30 asubuhi na kuanza kurusha risasi kwa kutumia silaha ya kivita aina ya AR.

Alisema watu wanne, walijeruhiwa kwa risasi ambapo mmoja wao ni kasisi wa sinagogi hilo.

"Inasikitisha, kwani mmoja kati yao alikufa kutokana na majeraha ya risasi," waathirika wengine watatu, akiwemo kasisi, wako katika hali nzuri," alisema Gore.

Alisema wengine waliojeruhiwa na risasi ni Waisraeli wawili, mtoto wa kike wa miaka nane na mjomba wake mwenye umri wa miaka 31 ambao walihamia San Diego miaka michache iliyopita wakitokea mji karibu na Ukanda wa Gaza, Israeli, ambao uliripotiwa kushambuliwa na roketi.

Gore alisema kuwa ofisa wa polisi wa doria mpakani aliyekuwa hayuko kazini alimuona mtu huyo akikimbia kutoka katika eneo la tukio la uhalifu huo ambapo alimlenga risasi lakini haikumpata.

Mkuu wa Polisi wa San Deigo, David Nisleit, alisema kuwa mshukiwa huyo aliwasiliana na polisi na baadae akajisalimisha kwa ofisa wa polisi San Diego ambaye alikuwa anaelekea katika eneo la shambulizi hilo la bunduki lilipotokea. Alisema mshukiwa huyo ana umri wa miaka 19 na anaishi San Diego. **VOA**

# Fao upotevu wa ajira

INATOKA UK.2

madai NSSF ni madai sahihi wengine wanadanganya na tunawakamata mara kwa mara."

Alisema wengi wanalalamika lakini madai yao yakichunguzwa kwa kina, inabainika si wanaostahili, lakini kwa wale wanaokutwa hawana matatizo yoyote, wanalipwa kwa wakati.

Alisema fao la upotevu wa ajira linatolewa kwa mtu mwenye taaluma ambaye ameachishwa kazi na atalipwa asilimia 33.3 ya mshahara wake, kama mbadala wa mshahara wakati anasubiri kupata kazi nyingine.

Kwa mujibu wa Erio, katika siku 23 za mwezi huu (Aprili 1-23), walilipa Sh. milioni 504.7 kwa wanachama waliodai fao hilo.

Aliongeza kuwa kuna changamoto kubwa ya wanaoachishwa kazi, akieleza kuwa mwanachama anaachishwa kazi leo, siku inayofuata anakwenda kwenye ofisi za mfuko kudai fao la upotevu wa ajira, jambo ambalo alisema siyo sahihi.

Alisema tangu mwaka jana hadi sasa, watu 15,258 wanalipwa fao la ukosefu wa ajira na Sh. bilioni 36.55 zimetumika.

Alisema kwa upande wa wanachama wasio na taaluma wanaochukua michango yao, 995 wameshalipwa, akifafanua kuwa ni wale ambao walikuwa wanafanya kazi za vibarua kwenye barabara, migodi na shambani.

**WAKATI GANI KUFUATILIA MAFAO?**

Alisema kwa mujibu wa utaratibu, mwajiri amepewa mwezi mmoja zaidi kuwasilisha michango ya wanachama, hivyo mwanachama kuachishwa kazi mwezi huo na kwenda kudai mwezi huo huo, michango yake inakuwa bado haijaufikia mfuko, mara nyingi mchango wa mwezi wake wa mwisho kuwa kazini.

"Inatakiwa ukiachishwa kazi, ukae mwezi mmoja ndiyo uende kwenye mfuko ili mchango wako uletwe, itakuwa rahisi kupiga hesabu kwa kutumia mshahara wa mwisho mwanachama alioachishwa nao kazi," alisema.

"Kwa mfano, michango ya mwezi wa nne itapelekwa mwezi wa tano, na malipo ya aliyepoteza ajira yataanza Juni mwaka huu.

"Mtu anataka akiachishwa kazi leo, basi kesho aje kwenye mfuko na siku inayofuata apewe fedha, utaratibu hauko hivyo maana ni lazima tupitie nyaraka na kufanya uchunguzi wa kina na baada ya kujiridhisha mhusika ataanza kulipwa kila mwezi."

# Askofu Pengo akemea ulevi

INATOKA UK.2

Askofu Pengo alisema wanasikia kwenye taarifa za habari, kuna maeneo ndani ya Tanzania ambayo saa moja asubuhi vijana huwa tayari wameshalewa na hawajui wafanye nini.

Alisisitiza kuwa wakati huo Mtume Petro alipata uwezo wa kutamka hivyo kwa sababu ya mazingira yake yalimruhusu kutamka.

"Tanzania mazingira tuliyonayo tunaweza kutamka hilo? Hilo linawezekana iwapo mazingira yote yamejengwa kwa kiwango, kama uwezekano huo unakuwa haupo, kuweza kutamka kitu cha aina hiyo mnahitaji serikali nzima ya Tanzania," alisema.

Akilizungumzia Jimbo Kuu la Mbeya na kanisa kwa ujumla, Askofu Pengo alisema watafanikiwa katika majukumu makubwa waliyopewa, iwapo watatambua, kusifia na kutukuza wema na mambo mazuri yanayofanywa na watu wengine hata kama siyo wakatoliki.

"Ni sharti tutambue kwamba lililo jema linatoka kwa Mungu na uvuvio wa Roho Mtakatifu, hatuwezi tukambeza Roho Mtakatifu kwa kumfunga kwenye sheria zetu, lazima tumwache atende kazi zake na zinapotokea kazi njema, tuwe tayari kuzitambua na kuzikiri kwa dhati," alisema.

"Ni dhambi peke yake inayoweza kutupatia sababu ya kubaguana, kutupatia sababu ya kufanya hili siyo jema, hili halifai, lakini siyo katika ule wema wa matendo.

## Waziri aipa maagizo TPDC

INATOKA UK.3

kiwanda cha Coca Cola.

Dk. Kalemani pia aliwataka TPDC kwenda kuwahamasisha wamiliki wa Mabasi yaendayo Haraka (UDART), pamoja na daladala kuanza kutumia magari yanayotumia gesi badala ya mafuta, kwani gharama zake ni kidogo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Mhandisi Kapuulya Musomba, alisema baada ya miezi sita wakazi 200 wanaishi eneo la Mikocheni watakuwa wameshaunganishwa na gesi asilia majumbani.

Alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo katika usambazaji wa gesi asilia ni makazi ya Jiji la Dar es Salaam kutokupimwa, pamoja na wakazi wengi kutokuwa tayari kutoa maeneo yao kwa ajili ya kupitisha miundombinu ya gesi.

Hadi sasa nyumba 24 za wananchi katika maeneo ya Mikocheni na UDSM wameshasambaziwa gesi asilia.

Usambazaji huo umefanikiwa baada ya kazi hiyo kuanza mwaka jana kwa kutoa gesi kwa bomba dogo katika kituo cha Ubungo kwenda kwenye maeneo husika.

## CAG abaini kuchelewa miradi shule

INATOKA UK.3

anaongeza kuwa ucheleweshaji huo pia unawazuia wananufaika kufurahia faida za mradi zilizokusudiwa kwa wakati uliopangwa na kusababisha hatari ya kuongezeka kwa gharama za mradi.

"Mradi wa ukarabati wa Shule za Sekondari Azania na Jangwani wenye thamani ya Sh. 2,418,240,784 unaelezwa kuchelewa kwa mwaka mmoja wakati mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Ihungo wenye thamani ya Sh. 10,488,414,429, ulichelewa kwa miaka miwili," CAG Assad anabainisha.


Prof. Assad anabainisha kuwa changamoto za kimuundo katika miradi hiyo kuwa ni mabomba kutosimikwa vizuri ardhini kwa makosa ya awali ya kiusanifu na makosa ya kitafiti ya kijiolojia, ikibainika urefu wa mabomba kukadiriwa chini ya mahitaji.

Anasema amebaini changamoto nyingine ni makandarasi wasio na uwezo, upungufu wa fedha, uwezo usioridhisha wa timu ya kiufundi, ukosefu wa zana/vifaa, upungufu katika ununuzi, ongezeko la muda wa kumaliza kazi usiotosheleza, kutokufuata matakwa ya mkataba, serikali kutokutoa fedha za kutosheleza na wakandarasi kutokufanya kazi kutokana na kutolipwa fedha zao.




**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**



# TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/03/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | Robo ya Mwaka/ wa sasa 31/03/2019 | Robo ya Mwaka/Uliopita 31/12/2018 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| Fedha Taslimu | 467,156 | 213,096 |
| Salio katika benki kuu ya Tanzania | - | - |
| Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| SALIO KATIKA BENKI NYINGINE NA TAASISI ZA FEDHA | 1,420,116 | 962,927 |
| Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| Miamala baina ya matawi | - | - |
| Bili zilizofikiwa | - | - |
| Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| Mikopo halisi iliyopo | 2,613,421 | 2,947,788 |
| Mali nyingine | 365,954 | 213,637 |
| Uwekezaji wa hisa | - | - |
| Akaunti za udhamini | - | - |
| Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 166,023 | 165,672 |
| **JUMLA YA MALI** | 5,032,670 | 4,503,120 |
| | - | - |
| **DHIMA** | | |
| Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| Amana za wateja | 1,983,285 | 1,092,657 |
| Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | | |
| Amana Maalum | - | - |
| Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | - |
| Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| Dhima nyingine | 441,235 | 318,121 |
| Madeni | 263,128 | 783,465 |
| **JUMLA YA DHIMA** | **2,687,648** | **2,194,243** |
| **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2,345,022** | **2,308,877** |
| **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| Mtaji wa hisa uliolipwa | 4,501,107 | 4,498,358 |
| Akiba ya mtaji | (2,360,795) | (2,468,330) |
| Mapato yaliyobakizwa | 43,208 | 105,046 |
| Faida(hasara)ya kipindi husika | 145,657 | 146,267 |
| Akaunti nyingine za mtaji | 15,845 | 27,536 |
| Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,345,022** | **2,308,877** |
| Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| Mikopo chechefu | 63,717 | 90,145 |
| Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 65,219 | 57,058 |
| Mali nyingine chechefu | - | - |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 47% | 51% |
| Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 0% | 3.1% |
| Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 132% | 270% |
| Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 52% | 65% |
| Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 80% | 87% |
| Ongezeko la Amana | 82% | -74% |
| Ongezeko la mali | 12% | 2% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/3/2019

(Kiasi kwa shilingi maelfu)

| | | Robo ya mwaka wa sasa 31/03/2019 | Robo ya mwaka linganishi(Mwaka uliopita ) 31/03/2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31/03/2019 | Limbikizo la mwaka linganisha (mwaka uliopita) 31/03/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato yariba | 157,548 | 92,773 | 157,548 | 92,773 |
| 2. | Gharama za riba | (4,582) | (15,859) | (4,582) | (15,859) |
| 3. | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **152,966** | **76,914** | **152,966** | **76,914** |
| 4. | Madeni viza yaliyopitwa | | | | |
| 5. | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (5,565) | (2,492) | (5,565) | (2,492) |
| **6.** | **Mapato yasiyo ya riba** | **38,246** | **86,507** | **38,246** | **86,507** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 38,246 | 86,507 | 38,246 | 86,507 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | - | - | - | - |
| **7.** | **Gharama zisizo na riba** | **(142,439)** | **(144,330)** | **(142,439)** | **(144,330)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (79,813) | (78,805) | (79,813) | (78,805) |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (62,626) | (65,525) | (62,626) | (65,525) |
| 8. | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **43,208** | **16,599** | **43,208** | **16,599** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | (12,962) | (4,980) | (12,962) | (4,980) |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **30,246** | **11,619** | **30,246** | **11,619** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 11 | 15 | 11 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.01 | 0 | 0 | 0 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.9% | 0.8% | 0.9% | 0.8% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.8% | -1% | 2% | -1% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 74% | 88% | 74% | 88% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8% | 5% | 8% | 5% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31/03/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/03/2019 | Robo Mwaka iliyopita 31/12/2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/3/2019 | Limbikizo la mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) 31/3/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 43,208 | 96,101 | 43,208 | 16,599 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | (1,840) | 10,534 | (1,840) | (710) |
| | - Hasara Katika Mali | 7,325 | 48,017 | 7,325 | 26,325 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 334,367 | (1,034,555) | 334,367 | 590,099 |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| | - Mabasiliko halisi katika amana | 890,628 | (3,187,914) | 890,628 | (1,707,869) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 123,114 | 107,625 | 123,114 | 12,669 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (152,317) | 16,902 | (152,317) | (23,259) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji** | **1,244,485** | **(3,943,290)** | **1,244,485** | **(1,086,146)** |
| II: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - | - | |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | (3,347) | (111,242) | (3,347) | -15,189 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | | | - | |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | 0 | 0 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | |
| | Mengineyo (Bainisha) | | | - | 0 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(3,347)** | **(111,242)** | **(3,347)** | **(15,189)** |
| III: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 2,750 | 3,388,222 | 2,750 | 20,446 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - | - | |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | (520,337) | (250,440) | (520,337) | (659,104) |
| | Mengnineyo | (12,301) | (72,364) | (12,301) | (24,136) |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(529,888)** | **3,065,418** | **(529,888)** | **(662,794)** |
| IV: | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslilmu | 711,250 | (989,114) | 711,250 | (1,764,129) |
| | Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/Mwaka | 1,176,022 | 2,165,136 | 1,176,022 | 2,165,136 |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/Mwaka** | **1,887,272** | **1,176,022** | **1,887,272** | **401,007** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 31/03/2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa | 4,498,358 | 0 | -2,363,284 | 2,836 | 27,536 | 143,431 | 2,308,877 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 43,208 | | | | 43,208 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 2,750 | | | | 0 | | 2,750 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | -9,280 | 9,280 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 11,691 | | -11,691 | | 0 |
| Mengineyo | | | 77 | | 0 | -9,890 | -9,813 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,501,108 | 0 | -2,317,588 | 12,116 | 15,845 | 133,541 | 2,345,022 |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | 1,110,136 | 0 | -2,498,748 | 112 | 18,415 | 0 | -1,370,085 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 105,046 | | | | 105,046 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | 0 | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 3,388,222 | | | | 0 | | 3,388,222 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | -2,724 | 2,724 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | -9,121 | | 9,121 | | 0 |
| Mengineyo | | | 42,263 | | 0 | 143,431 | 185,694 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,498,358 | 0 | -2,363,284 | 2,836 | 27,536 | 143,431 | 2,308,877 |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha ,sera za uandaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| | Tarehe |
|---|---|
| Mugwagi Steven<br>**Mtendaji Mkuu** | 29/4/2019 |
| Anthony Bichakila<br>**Mkuu wa fedha** | 29/4/2019 |

**Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.**

| | Tarehe |
|---|---|
| Rajab Mmunda<br>Mwenyekiti wa bodi | 29/4/2019 |
| Elibariki Masuke<br>Mjumbe wa bodi | 29/4/2019 |

215199102

# NEYMAR: MAKINDA WANAONGEA SANA




**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar amewashutumu baadhi ya wachezaji wenzake vijana baada ya kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa 'Coupe de France', dhidi ya Rennes kwa penalti 6-5, baada ya sare ya kufungana 2-2 ndani ya dakika 120.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alifunga bao la pili kwa PSG baada ya Dani Alves kufunga la kwanza, lakini Rennes walipigana na kusawazisha kupitia kwa Presnel Kimpembe aliyejifunga na bao la Mexer, kabla ya kushinda penalti baada ya Christopher Nkunku kukosa mkwaju wake.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Neymar aliwashauri wachezaji wenzake vijana kuwasikiliza zaidi wachezaji wakongwe na wenye uzoefu katika kikosi hicho.

"Tunahitaji kuwa wanaume kamili kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, tunatakiwa kuungana zaidi," alisema. "Nimewaona wachezaji wengi vijana ambao hawasikilizi, lakini wanaongea mno.

"Wanatakiwa kusikiliza zaidi kuliko kuongea. Wakati mwingine wachezaji wenye uzoefu wanapozungumza, na wao wanajibu. Kocha mwenyewe akizungumza nao wanajibu. Hii si staili ya timu, hatuwezi kufika mbali.

"Tuna uzoefu wa kutosha, hivyo wanatakiwa kutuheshimu, watusikilize zaidi. Nilikuwa nafanya hivyo nilipokuwa kijana zaidi."

## Asensio aziweka sawa Liverpool, Bayern

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inajiandaa kusikiliza ofa kwa Marco Asensio majira haya ya joto.

Na Gazeti la El Confidencial, limeeleza kuwa Real inajiandaa kumweka sokoni ikihitaji euro milioni 150 hadi 180.

Hata hivyo, Liverpool, Juventus na Bayern Munich zote zinamfukuzia na kuwekwa kwake sokoni kutaziwezesha kuanza mbio rasmi.

Asensio amejikuta akikosa namba katika nafasi ya kiungo kutokana na ubora wa Vinicius Junior na Brahim Diaz msimu huu.

Kama ilivyokuwa wiki moja iliyopita, wakala wake, Horacio Gaggioli alifunguka: "Zaidi ya mwaka uliopita kulitolewa ofa ya euro milioni 150 na euro milioni 180, lakini Madrid haikutaka kusikiliza ofa hiyo.

"Mara zote kuna klabu kubwa zinavutiwa na Marco, zinaangalia kama anataka kuondoka, kitu ambacho ni kawaida mchezaji."





## *Leicester City yaififisha Arsenal 4 -bora EPL*

**LONDON,** England

MATUMAINI ya Arsenal kumaliza nafasi nne za juu Ligi Kuu England, yameendelea kufifia baada ya jana kukubali kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya wenyeji wao, Leicester.

Arsenal ingepigwa mabao mengi zaidi kama si umakini wa kipa Bernd Leno wakati Leicester ikiwa tayari inafurahia umiliki mpira kwa asilimia 72 wakati huo Ashley Maitland-Niles akiwa ameshaonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyoambatana na nyekundu katika dakika ya 36 kufuatia kumchezea rafu James Maddison.

Youri Tielemans ndiye aliyefungua akaunti ya mabao kwa 'Mbweha' hao katika dakika ya 59 kabla ya Jamie Vardy kutupia mawili katika dakika ya 86 na (90+5). Arsenal inabaki katika nafasi ya tano, hata hivyo uwapo wao hapo ukiwa ni kabla ya mechi kati ya Manchester United na Chelsea jana jioni.

Manchester ilikuwa na nafasi ya kuishusha Arsenal hadi mtaa wa sita endapo jana jioni imepata matokeo dhidi ya Chelsea iliyopo nafasi ya nne. Kwa upande mwingine matokeo hayo ya jana yameipandisha Leicester hadi nafasi ya nane, ikiwa pointi tatu nyuma ya Wolves inayoshika nafasi ya saba.

Hata hivyo, mambo yangeweza kuwa tofauti kama Alex Iwobi asingepiga shuti lake moja kwa moja kulenga miguuni kwa kipa Kasper Schmeichel katika dakika ya 35.

Arsenal sasa inajiandaa na mechi ya nusu fainali ya Europa League dhidi ya Valencia Alhamisi wakati Leicester City ikijiandaa na mchezo dhidi ya Manchester City.

# ZIDANE AFUNGUKA HAZARD, NEYMAR MADRID



**MADRID,** Hispania

KOCHA Zinedine Zidane, amevunja ukimya na kueleza kuwa kuna uwezekano wa kuwakutanisha Neymar da Silva Santos Junior anayekipiga Paris Saint-Germain, Eden Hazard anayeitumikia Chelsea na Gareth Bale katika kikosi chake cha Real Madrid.

Zidane ameyasema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tetesi za usajili wa donge nono unaotarajiwa kupitia kwake, katika njia ya kuiongezea makali ya washambuliaji klabu hiyo.

Alipoulizwa kama Neymar anaweza kukamilisha ndoto yake ya kucheza katika upande mmoja na Hazard nchini Hispania, Zidane aliwaambia waandishi wa habari, "ndiyo. Tuna wachezaji wengi wazuri wanaotaka kuja hapa na kuichezea Real Madrid. Hiyo inawezekana lakini tuwe wavumilivu tuone kitakachotokea."

Katika hatua nyingine, Zidane amekanusha tetesi kuwa ujio wa Hazard kwenye klabu hiyo utaiweka rehani nafasi ya Gareth Bale. Alisema tetesi kuwa wachezaji hao hawawezi kucheza pamoja ni upuuzi.

"Huo ni upuuzi, kila mchezaji mzuri duniani anaendana na mwenzake. Walisema mambo kama hayo hayo kwangu mimi na (Youri) Djorkaeff, ni upuuzi tu," aliongeza.

Miamba hao wa Santiago Bernabeu wanadaiwa kuwa kwenye wakati mgumu wa kuupata mbadala wa Cristiano Ronaldo, hali iliyozua tetesi nyingi kwa washambuliaji wengi wazuri kwa madai kuwa huenda wakaingia kwenye orodha ya mkwanja atakaokabidhiwa Zidane. Kylian Mbappe pia anatajwa kwenye orodha hiyo.

## Norwich City yapanda Ligi Kuu England

**LONDON,** England

KLABU ya Norwich City, imefanikiwa kurudi kwenye Ligi Kuu ya England baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Blackburn Rovers kwenye dimba la Carrow Road.

Kuelekea kwenye mchezo huo, kocha Daniel Farke alitambua kwamba anatakiwa kuepuka kipigo ili kuweza kupata nafasi hiyo.

Na mabao kutoka kwa Marco Stiepermann na Mario Vrancic yakifungwa ndani ya dakika 20, yaliisaidia Norwich kupata ushindi huo na kufanikiwa kurudi tena kwenye Ligi Kuu.

Blackburn walipata bao lao kupitia kwa Lewis Travis, lakini halikutosha kuwafanya waondoke na pointi tatu.

Norwich ambayo imecheza Ligi Kuu ya England mara kadhaa na kushuka, sasa inatambua wazi kwamba, kazi waliyo nayo mbele yao ni kuhakikisha wanaboresha kikosi chao tayari kwa ajili ya msimu ujao.

Kocha Farke alisema mara baada ya mchezo huo kuwa kilichopo mbele yao sasa ni Ligi Kuu tu.

"Tupo Ligi Kuu, hili ndio jambo ninalolijua kwa sasa, mengine yatafuata," alisema.



# Messi atwaa ndoo ya 10 La Liga



**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi, amejiwekea ufalme wa aina yake baada ya usiku wa kuamkia jana kuiwezesha timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga hiyo ikiwa ni mara ya 10 kwake.

Barcelona imetwaa ubingwa huo wakati zimebakia mechi tatu kumalizika kwa michuano hiyo ya Ligi Kuu msimu huu ambayo inafikia tamati mwezi ujao.

Messi alifunga bao katika dakika ya 62 akiwa ameingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Phillipe Coutinho kwenye mchezo huo dhidi ya Levante na kuwapa miamba hao wa Katalunya ubingwa wa La Liga.

Kwa ushindi huo Barcelona haitaweza kufikiwa na Atletico Madrid iliyopo nafasi ya pili ambayo ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mchezo wa mapema.

Ubingwa huo sasa umemfanya Messi kuingia kwenye rekodi maalum ya kuwa mchezaji wa kwanza kutwaa mataji 10 ya La Liga.

Messi ambaye amedumu katika klabu hiyo kwa muda mrefu, amefanikiwa kutwaa taji hilo la 10 la La Liga kukiwa hakuna mchezaji yeyote asiye kuwa na asili ya Hispania kuwahi kuweka rekodi ya kutwaa taji hilo mara 10.

Barcelona wametangazwa mabingwa wa michuano hiyo wakiwa wana michezo mitatu mkononi.

Pamoja na hayo, Messi amewejiwekea ufalme mwingine wa kivyake kwa kucheka na nyavu ndani ya La Liga baada ya kufikisha jumla ya mabao 34 kwa sasa kwenye ligi hiyo huku akimuacha mbali mpinzani wake wa Real Madrid, Karim Banzema mwenye mabao 21.

Messi kwa sasa katika Ligi Kuu tano kubwa za Ulaya, anafuatiwa na Kyllian Mbappe ambaye amefunga mabao 30 akiwa na klabu yake ya PSG ya Ufaransa.

Messi amecheza dakika 2485 na ana wastani wa kupachika bao moja kila baada ya dakika 75 akiwa ndani ya uwanja huku akitoa jumla ya pasi za mwisho 13 kwa timu yake ambayo imefunga jumla ya mabao 83.

Upande wa Benzema yeye amecheza dakika 2795 akiwa na wastani wa kufunga bao moja kila baada ya dakika 133 akiwa uwanjani na timu yake imefunga jumla ya mabao 59.

Kwa upande wa Cristiano Ronaldo ambaye yupo Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akikipiga Juventus ametupia jumla ya mabao 19 na ametoa pasi 8 za mabao huku akicheza jumla ya dakika 2329 ana wastani wa kufunga bao moja kila baada ya dakika 123.

# DONDOO ZA SO
## MAGAZETI YA ULA



# RONALDO AMUWAHI MESSI MABAO 600

## ●●● Ni mchezaji pekee aliyeshinda mataji ya Ligi Kuu katika Ligi tatu tofauti kubwa Ulaya...

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo, amefunga bao lake la 600 kwa ngazi ya klabu na la 20 msimu huu wakati Juventus ikitoka sare ya kufungana 1-1 dhidi ya Inter Milan Jumamosi.

**Na kwa idadi hiyo, Ronaldo amemtangulia mpinzani wake, Lionel Messi kufikisha mabao 600, kwani hadi sasa nyota huyo wa Barcelona ameshatupia jumla ya 598 akiwa na miamba hiyo ya Catalunya.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alifunga bao hilo akiwa ndani ya eneo la penalti akiunganisha pasi ya kisigino ya Miralem Pjanic na kufanya matokeo kuwa 1-1, baada ya Inter kutangulia kwa bao la Radja Nainggolan.

Juventus na Ronaldo tayari wameshatwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, lakini ilikuwa ni sehemu nyingine kwake kuweka rekodi ya aina yake katika upachikaji wa mabao.

Ronaldo katika kipindi chake pale Real Madrid, alifunga mabao 450 katika mashindano yote, pia akiwa amefunga mabao 118 wakati akiwa anaichezea Manchester United, matano akicheza katika klabu yake ya kwanza ya Sporting CP na sasa amefikisha mabao 27 aliyoifungia Juventus katika mashindano yote aliyoichezea.

Na katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ronaldo ameshafunga jumla ya mabao 126 ambayo ni zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye historia ya michuano hiyo, huku kwenye Klabu Bingwa Dunia akicheza na nyavu mara saba na mara mbili katika UEFA Super Cup.

Ronaldo, 34, ni mchezaji pekee aliyeshinda mataji ya Ligi Kuu katika Ligi tatu tofauti kubwa Ulaya, England, Hispania na Italia.

England alishinda mara tatu, La Liga mawili na moja Serie A na ameshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la Klabu Bingwa ya Dunia.

Juventus, ambao walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali na Ajax pia hawapo kwenye Kombe la Coppa Italia na wamebakisha mechi nne kumaliza msimu huu wa Ligi Kuu ya Italia.

## ZISIKUPITE

### POGBA AOMBA KUONDOKA UTD

KIUNGO wa Manchester United, Mfaransa Paul Pogba, ameiambia klabu yake hiyo kuwa anataka kujiunga na Real Madrid majira haya ya joto na tayari ameshakubaliana malipo yake na miamba hiyo. ***(AS - in Spanish)***

### KOULIBALY, INSIGNE RUKSA

KOCHA wa Napoli, Carlo Ancelotti amesema hatamzuia beki wa kati Msenegal Kalidou Koulibaly, 27- anayeripotiwa kuwindwa na Manchester United - na mshambuliaji Mtaliano Lorenzo Insigne, 27, anayehusishwa na Chelsea na Liverpool kama wanataka kuondoka majira haya ya joto. ***(Mail on Sunday)***

### PJANIC BEI JUU JUVE

PSG imetoa ofa ya pauni milioni 60.5 kwa kiungo wa Juventus, Bosnia na Herzegovina, Miralem Pjanic, 29, lakini miamba hiyo ya Serie A inataka pauni milioni 86 ili kumwachia. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### WENGER KUPEWA KAZI LYON

MIAMBA ya Ligue 1, Lyon, imefanya mawasiliano na kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger kuhusu kuchukua mikoba ya Bruno Genesio, ambaye ataondoka mwishoni mwa msimu. ***(L'Equipe - in French)***

### HAZARD, BALE KUCHEZA PAMOJA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema mshambuliaji wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29, na wa Chelsea, Mbelgiji Eden Hazard, 28, ambaye amekuwa akihusishwa na kutua Bernabeu, watakuwa pamoja katika timu moja. ***(Marca)***

### YAWATAKA MAGUIRE, VAN DIJK

Manchester City inataka kumsajili beki wa Leicester na England, Harry Maguire, 26, lakini 'Mbweha' hao wanataka pauni milioni 90 ili kumwachia. Kocha wa City, Pep Guardiola pia anavutiwa na beki wa Liverpool, Mholanzi Virgil van Dijk, 27. ***(Sun on Sunday)***

### JUVE, PSG KWA DE GEA

MABINGWA wa Italia, Juventus, wanaweza kujaribu kuipiku Paris St-Germain katika mbio za kumsajili kipa wa Manchester United na Hispania, David de Gea. ***(Le10 Sport - in French)***

### AWANIWA MARSEILLE, PSG

Paris St-Germain na Marseille zinavutiwa na kocha wa Newcastle, Rafael Benitez. ***(Sunday Mirror)***

### JUVE KUMVUNJIA POGBA BANKI

JUVENTUS inataka kumrejesha Paul Pogba Turin, lakini itapaswa kuwauza wachezaji watatu muhimu ili kumudu kumnunua nyota huyo wa Manchester United kwa euro milioni 130 anayothaminishwa nayo Mfaransa huyo. ***(Observer)***

### BIELSA KUACHANA NA LEEDS

KOCHA wa Leeds, Marco Bielsa anaweza kuondoka katika klabu hiyo ya Championship kama haitafanikiwa kupanda Ligi Kuu England, EPL. ***(Mail on Sunday)***

### ALLARDYE KUINOA INDIA

KOCHA wa zamani wa England, Sam Allardye anaweza kurudi katika kazi kimataifa kwa kuibukia kuinoa India. ***(Sunday Mirror)***

## Tulia Marathon 2019 zazinduliwa Mbeya

**Na Frank Monyo**

TAASISI ya Tulia Trust imezindua rasmi mbio za Mbeya Tulia Marathon 2019, zitakazofanyika Mei 4, mwaka huu katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kushirikisha makundi mbalimbali likiwamo kundi la walemavu na wazee.

Akizungumza na waandishi habari jana jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi huo, Balozi mpya wa Tulia Trust, Yvonne Cherry maarufu Monalisa, alisema katika mashindano ya mbio hizo fedha zitakazopatikana zitatumika katika kusaidia jamii katika nyanja ya elimu na afya.

"Pesa zitakazopatikana kwa watu kujisajili kushiriki katika mbio hizo zitatumika katika kuboresha sekta ya afya na elimu na hii si kwa Mbeya tu bali ni Tanzania nzima na katika mashindano ya mwaka huu yatakuwa na mvuto kwani makundi maalaum yatashiriki mbio hizo," alisema Monalisa

Aliongeza kuwa kutakuwa na mbio za kilomita 42 "Full Marathon", Kilomita 21 "Half' Marathon, ambazo gharama ya usajili wa ushiriki ni Sh. 30,000 kila kipengele na kwa mbio za kilomita tano na kilomita mbili ambazo zitakuwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, wazee na watoto gharama yake itakuwa ni Sh. 20,000 kwa kila kilometa.

Katika uzinduzi huo, walitambulishwa mabalozi wapya ambao ni pamoja msanii wa Bongo Fleva, Mwasiti na Mtangazaji Kennedy Urio maarufu Kennedy Remmedy.

Taasisi ya Tulia Tust Machi 3, mwaka huu ilifanikiwa kutoa msaada wa kwenda kupatiwa matibabu nchini India mwanafunzi Amos Gabriel ambaye alivunjika mgongo.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Simba | 27 | 22 | 3 | 2 | 57 | 11 | 69 |
| 3. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 11. Singida Utd | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 20 | 27 | 39 |
| 14. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 33 | 9 | 10 | 14 | 24 | 36 | 37 |
| 17. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 32 | 8 | 10 | 14 | 22 | 31 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# KITAMBI SASA APEWA MKATABA RASMI SIMBA



**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

BAADA ya kutoweka klabuni kwa madai ya kudai mkataba, hatimaye uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba umemkabidhi nakala ya mkataba kocha wake msaidizi, Dennis Kitambi (pichani), imeelezwa.

**Kitambi hakuonekana katika kikosi cha Simba baada ya kurejea jijini Dar es Salaam wakitokea Tanga walikokwenda kuivaa Coastal Union.**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili kuwa tayari wameshampa Kitambi nakala ya mkataba wake na mchakato huo ulichelewa kutokana na mwanasheria wa klabu kuwa nje ya nchi.

Magori alisema kuwa licha ya kuchelewa kumpa nakala hiyo, kocha huyo alikuwa akipata stahiki zake zote walizokubaliana kwa wakati ikiwamo kulipiwa nyumba na kupewa gari.

"Ila uamuzi wake huo haukuwa wa busara, haukuwa na afya kwa timu ambayo ilikuwa inakabiliwa na mechi ngumu za Kanda ya Ziwa, sasa ni juu yake," alisema kiongozi huyo.

Alisema chini ya utawala wake, Simba inajitahidi kufanya kazi kisasa licha ya kukutana na changamoto za hapa na pale huku ikijipanga kuboresha shughuli zote za utendaji za kila siku za klabu hiyo.

Magori alitarajia kuongoza kundi la mwisho la wachezaji wa Simba kurejea Dar es Salaam jana usiku tayari kuanza mazoezi ya kuwakaribisha JKT Tanzania katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru.




Ofisa Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Khamis Mussa (katika), akimkabidhi jezi kiongozi wa timu ya Mbuyuni, Rashid Maulid, katika hafla iliyofanyika Chake Chake Pemba. Anayeshuhudia makabidhiano hayo ni Mkuu wa Ufundi na Teknolojia wa Zantel, John Sicilima (kushoto). Timu sita zimepokea jezi kutoka Zantel katika mpango wa kampuni hiyo kuendeleza michezo visiwani hapa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Biashara Utd yaahidi kubaki Ligi Kuu*

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

IKIWA imebakiza mechi sita mkononi, uongozi wa Mkoa wa Mara na benchi la ufundi la Biashara United, umesema timu hiyo haitashuka daraja kama inavyodhaniwa na wadau wengi wa soka hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi mjini hapa, muda mfupi baada ya Biashara United kupata kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kutoka jijini Dar es Salaam.

Biashara United ina pointi 34 baada ya kucheza mechi 33 na katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko katika nafasi ya 19 wakati African Lyon inayoburuza mkia imejikusanyia pointi 22.

Akizungumza na gazeti hili, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alisema timu yao ina uwezo wa kufanya vema katika mechi zilizobakia na hiyo imeonekana baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye mchezo uliopita dhidi ya Simba licha ya kupoteza.

Malima alisema hawajakata tamaa na wataendelea kujipanga kwa kuwaandaa vema wachezaji wao kwa kurekebisha makosa yaliyoonekana na hatimaye kuingia wakiwa imara zaidi pale watakapoikaribisha Lipuli FC mapema wiki ijayo.

"Simba ni timu kubwa, ina wachezaji wazoefu, wametumia vizuri nafasi walizopata, sisi tumeona makosa yetu, tutajiimarisha ili tupate ushindi katika mechi zilizobakia hapa nyumbani na moja ya ugenini," alisema kiongozi huyo.

Amri Said, kocha mkuu wa timu hiyo, aliliambia gazeti hili kuwa bao la mapema liliwaondoa mchezoni wachezaji wake ambao pia hawakuwa na umakini.

"Simba walicheza vema kuliko sisi, waliweza kutawala mpira kwa kiwango kikubwa, wachezaji wangu hawakuwa katika ubora wao, hasa upande wa viungo na mabeki hawakucheza vizuri, ila bado nafasi tunayo," alisema kocha huyo ambaye alitua Biashara United akitokea Mbao FC.


Aliongeza kuwa ana matumaini ya kuendelea kubaki katika ligi hiyo kutokana na wachezaji wake kuimarika na kucheza soka la ushindani tofauti na alivyowakuta wakati anaichukua timu hiyo.

# Michezo

Jumatatu Aprili 29, 2019
Nipashe



Neymar: Makinda wanaongea sana HABARI UK.28



Youri Tielemans (kulia jezi ya bluu), akiunganisha nyavuni kwa kichwa krosi ya James Maddison na kuipa Leicester bao la kuongoza wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0, katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal iliyopigwa Uwanja wa King Power jana. **HABARI UK. 29**

## Aussems: Kazi haijaisha Simba

**Na Somoe Ng'itu,** MUSOMA

BAADA ya kuvuna pointi tisa kutoka timu nne za Kanda ya Ziwa, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema "bado hatujamaliza kazi".

Simba ambao ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa wamebakiza viporo vitano kufikia idadi sawa za mechi na vinara wa ligi hiyo, Yanga wenye pointi 74 baada ya kushuka dimbani mara 32.

Aussems aliliambia gazeti hili mjini hapa kuwa bado kikosi chake kinahitaji kushinda mechi zote za ligi hiyo zilizosalia ili kujiimarisha katika mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia ambao bado uko wazi.

Kocha huyo alisema mechi zote wanazocheza zina ushindani na hiyo inatokana na kila timu bado haijakaa katika nafasi salama kwenye msimamo kwa kuzingatia malengo waliyonayo.

"Bado tuna kazi ya kufanya, mechi zote ni ngumu, ligi bado ina ushindani, hakuna mechi rahisi, kila timu inahitaji ushindi ndio maana hakuna anayekata tamaa mpaka filimbi ya mwisho inapopigwa, tunataka kushinda kila mechi iliyopo mbele, " alisema Mbelgiji huyo.

Aliongeza kuwa ameridhishwa na kiwango cha kila mchezaji aliyecheza katika mechi zote nne walizocheza kuanzia dhidi ya Kagera Sugar, Alliance FC, KMC FC na Biashara United iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini hapa.

Naye nahodha wa timu hiyo, John Bocco, alisema ushindi wa mechi tatu mfululizo waliopata ulitokana na wachezaji wote kujituma na kufahamu wanahitaji kutimiza malengo ya kushinda taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa huu unaoelekea ukingoni.

# Yanga, Azam ni zaidi ya vita

### ●●● Rekodi zilipokutana zinatisha, Simba yaziongezea presha huku kila moja...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA leo itakuwa na kibarua kizito kwenye Uwanja wa Uhuru ikipambana dhidi ya Azam kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

**Utakuwa ni mchezo wa 21 kwa timu hizo, tangu zilipoanza kukutana pale Azam ilipopanda Ligi Kuu na kucheza kwa mara ya kwanza msimu wa 2008/09.**

Tayari timu hizo zimekutana mara 20 kwenye mechi mechi za Ligi Kuu, huku kila timu ikishinda mara sita na zikitoka sare mara nane.

Mechi ya leo itakuwa ni zaidi ya mechi ya kawaida ya Ligi Kuu kwani kuna vitu vingi ambavyo timu hizo zitafanya wachezaji kuingia uwanjani kwa lengo moja tu la kuhitaji ushindi.

Ushindi mfululizo inaoupata timu ya Simba utasababisha mechi ya leo kuwa kali kwani zote zitakuwa na lengo moja tu kutaka pointi tatu ili kukabiliana na mnyama anayeonekana kutoshikika.

Yanga itataka ushindi kwa udi na uvumba ili kufikisha pointi 77 na hili litakuwa ni jaribio lake la kutaka kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa ubingwa huku ikiombea mabaya Simba kwenye mechi zake zilizosalia.

Sare yoyote au kufungwa, kutaiweka Yanga kwenye mazingira magumu zaidi kupata ubingwa msimu huu, kwani kwa sasa ina pointi tano tu zaidi ya mahasimu wao, Simba.

Kwa upande wa Azam, ushindi kwake utakuwa umeifanya kuifukuza Simba, kwani timu hiyo imeshakalia nafasi ya pili ambayo 'Wanalambalamba' walikuwa wanaimiliki kwa muda mrefu.

Azam, yenye pointi 66, itataka kufikisha pointi 69 na kuifikia Simba, ikiombea mabaya kwenye mechi zake zinazofuata.

Kwa hapo utaona jinsi gani mechi ya leo itakavyokuwa kali na ya kusisimua, kwani hakuna timu ambayo kwake sare itamuweka salama zaidi ya ushindi.

Kingine ambacho mashabiki wa soka nchini watakachokishuhudia ni mastraika hatari na tegemeo kwa Yanga msimu uliopita na mingine nyuma, Donald Ngoma na Obrey Chirwa akicheza dhidi ya timu yao ya zamani kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu.

Wachezaji hao walicheza dhidi ya kikosi cha pili cha Yanga kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Mara ya mwisho kukutana baina ya timu hiyo kwenye Ligi Kuu msimu wa 2017/18, Azam iliifumua Yanga mabao 3-1 kwenye mechi ya mwisho ya kufunga dimba la ligi msimu uliopita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >